

**Lulu** apanga jinsi atakavyolea watoto

UKURASA 20



**Ronaldo** yupo sana Juventus - Pepe

UKURASA 21


**MAISHA** Nipashe Baba, Mama na Mwana Jumapili



Hana adabu, mzazi unahusika



MAISHA NI NYUMBA
Tambua haya unapofunga kamba za nguo nyumbani



HARUSI



Raha ya ukwaju katika urembo

UKURASA 9

Jumapili Aprili 18, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0580554

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US

MAHOJIANO MAALUM:

# Waziri wa JPM afichua siri alivyokwepa ufisadi

UKURASA 4

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

**WAZIRI, WANANCHI WAPEWA SIKU 90 KUONDOKA HIFADHINI**

MAMLAKA ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), imetoa notisi ya siku 30 kwa...

UKURASA WA 5

**MCHUMI KORTINI TUHUMA ZA KUSABABISHA HASARA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Singida...

## Baba adaiwa kuua mama, mtoto kwa wivu wa mapenzi

UKURASA 2



Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Samia Suluhu Hassan, akikagua gwaride maalum lililoandaliwa na maofisa wanafunzi wa JWTZ kabla ya kuwatunuku kamisheni za kijeshi, katika viwanja vya Ikulu ya Chamwino, Dodoma jana. **PICHA: IKULU**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## Wadau watoa maoni kamati tathmini kikokotoo mafao

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA KAZI KAZI KWA MWADUI LEO UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Baba adaiwa kuua mke na mtoto wake

**Na Restuta Damian,** MULEBA

JOACHIM Rwegasira (45), mkazi wa kijiji cha Buhanga, Muleba mkoani Kagera, anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani hapa kwa tuhuma za mauaji ya mke wake, Rosemary Joachim mtoto wa mwaka mmoja, Joines Joachim.

Rweasira (45) anatuhumwia kufanya mauaji hayo kwa madai kwamba mke wake alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na jirani yake.

Baada ya mauaji hayo, mtuhumiwa alijaribu kujiua kwa kujijeruhi sehemu mbalimbali za mwili zikiwamo tumboni na shingoni.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Maketi Msangi, alithibitisha kutokea tukio hilo Aprili 16, mwaka huu, majira ya 9:00 jioni nyumbani kwa wanandoa hao.

Msangi alisema chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa mapenzi kwa madai kwamba Rosemary, ambaye ni mke wake, alikuwa na uhusiano na jirani yake na kudhaniwa kuwa mtoto huyo aliyemuua hakuwa wake.

"Akiwa mtaani watu walimwambia kuwa mtoto huyo siyo wake ni wa jirani yake na alipeleka malalamiko ngazi za kijiji kabla ya kufanya mauaji hayo," alisema Msangi

Kamanda Msangi alisema baada ya mauaji hayo, mtuhumiwa alijijeruhi tumboni na shingoni kwa kutumia kitu chenye ncha kali kwa lengo la kutaka kujiua.

Alisema uongozi wa kijiji na Polisi wilayani Muleba walikuta miili ya marehemu imelazwa chumba kimoja na yeye kukutwa sebuleni akiwa na hali mbaya.

Msangi alisema mtuhumiwa anaendelea na matibabu katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Rubya akiwa chini ya ulinzi wa polisi.



Aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Dk. Edward Hoseah, akila kiapo cha kuwa Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), jijini Arusha jana, baada ya kushinda uchaguzi uliofanyika, juzi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Wadau watoa maoni kamati kikokotoo

**Na Waandishi Wetu**

HATUA ya serikali kuunda kamati mahususi kushughulikia dosari zilizojitokeza katika kanuni mpya za ulipaji mafao kwa wastaafu, wadau wamepongeza na kutaka mchakato huo uhusishe wadau wote muhimu ili kuepuka malalamiko baadaye.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, baadhi wameishauri kamati hiyo kujielekeza kufanya utafiti wa kina na kuja na majibu kuhusu hasara za awali kabla ya kuanza kwa kikokotoo kipya.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), Dk. Paul Loisulie, alisema endapo kutakuwa na marekebisho, ni vyema yakahusisha wadau wote muhimu ili kuepusha malalamiko.

"Wadau si TUCTA (Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania) peke yao maana serikali huwa inawashirikisha wao tu ikiamini watu wote wamehusishwa. Vipo vyama vya wafanyakazi nje ya TUCTA, asasi za kiraia, na wadau wengine," alisema.

Pia alishauri serikali ipate maoni ya watu waliostaafu miaka ya karibuni na miaka ya nyuma, ili kujua hali halisi ya maisha yao baada ya kustaafu na kwamba hiyo itasaidia kutengeneza kikokotoo rafiki. Alishauri pia serikali itoe muda wa kutosha kujadili ili kuepuka kuburuzana.

**MGAYA AIBUKA**

Katibu Mkuu Mstaafu wa TUCTA, Nicholaus Mgaya, alipongeza hatua ya serikali kuunda kamati hiyo na kushauri kuwa inapaswa kushirikisha utatu wa vyama vya wafanyakazi, vyama vya waajiri na serikali ambao wanapata mwafaka wa uhalisia wa kikokotoo hicho kipya.

Alisema kuundwa kwa kamati hiyo kutasaidia kutoa mapendezo ya nini kiwapo na kipi kisiwapo kwa maslahi ya wastaafu wote, baada ya hapo.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Mawasiliano na Uchukuzi (COTWU) Kanda ya Tabora, Oscar Polepole, aliitaka kamati iliyoteuliwa wastaafu kutenda haki kwa kuwafikia wafanyakazi wa kanda mbalimbali ili kupata maoni yao kabla ya kufanya marekebisho yaliyokusudiwa.

"Wafanyakazi wengi tuliipinga hii kanuni mpya kwa kuwa haina manufaa kwa mstaafu. Tuliandamana kuipinga na Rais John Magufuli alisitisha utekelezaji akatoa muda hadi mwaka 2023 kamati iwe imetoa maboresho mapya baada ya kusikiliza maoni ya wadau," alisema Polepole.

**UTAFITI UFANYIKE**

Mhadhiri Mwandamizi wa Kitivo cha Ushirika na Maendeleo ya Jamii ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MOCU), Dk. Gervas Machimu, alisema ili kuwasaidia wastaafu, kamati maalum iliyoundwa inapaswa kujielekeza kufanya utafiti wa kina na kuja na majibu kulikuwa na hasara gani kabla ya kuanza kwa kikokotoo kipya.

Alisema kinachotakiwa kufanywa ili kuridhiwa na wanachama, ni kuja na maboresho yatakayozingatia hasara kwa pande zote mbili, kwa maana ya faida kwa wanachama na mfuko.

Dk. Machimu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taifa wa Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (SCCULT Ltd-1992), alisema: "Nakubaliana moja kwa moja na uamuzi wa serikali kuunda kamati hiyo kwa sababu watapunguza machungu ya wachangiaji wa mfuko na maumivu ya utaratibu huu uliotaka kutumika kabla ya kuundwa kamati.

"Kamati itatusaidia kuja na faida na hasara ya nini kilichokuwapo katika kikokotoo kilichokuwa kikipigiwa kelele kwa muda mrefu na kitakachopendekezwa na kamati kwa sasa," alisema.

Ofisa Mifugo wa Bodi ya Nyama, Geofrey Kakuru, alisema ni vyema kanuni hizo za Kikokotoo zifanyiwe marekebisho ili wastaafu wapewe kwa mkupuo asilimia kubwa.

Alisema kiasi cha mafao yanayobaki ndiyo waingize kama mshahara ndani ya miaka ilioanishwa katika kanuni hiyo huku akibainisha kuwa mfanyakazi anapostaafu nguvu kazi zinakuwa zimedhoofika, hivyo anapolipwa mafao yake anakwenda kufanya shughuli za maendeleo.

"Ukimpatia asilimia 25 inakuwa ndogo sana kwake. Anaweza kupoteza maisha kabla hata hajaipata hiyo. Ni vema serikali iangalie namna ya kurekebisha kanuni hiyo iwe kama zamani," alisema.

Naye Katibu wa Chama cha Wafanyakazi Bandari Mkoa wa Dar es Salaam, Hassan Ahmedy, alisema wafanyakazi wanapostaafu husukani katika nchi za Afrika, wanakuwa wamechoka, hivyo uwezekano wa kuishi muda mrefu ni mdogo kulingana na uhalisia wa maisha ya sasa.

"Mtu anapostaafu inatakiwa apate ikiwezekana asilimia 75 ya mafao yake ili kama anataka kukamilisha mipango yake afanye hivyo bila kipingamizi na 25 inayobaki ndiyo apewe kama mshahara," alisema.

Erasto Mgeni, mkazi wa Njombe, alisema: "Wananchi waliichukia serikali kwa sababu ya kukosa haki yao, ililikua ni jambo la ajambo na la kuumiza na kufedhehesha kwa hiyo tuitakie kila la kheri kamati iliyoundwa ije na majibu ambayo yatakuja kurekebisha changamoto hiyo".

Mwanasheria wa Shirika la Haki za Binadamu wilayani Kahama, Pius Mpondi, alisema marekebisho ya kikokotoo yatasaidia watumishi wengi kujikkwamua kiuchumi.

Mpondi alisema ikiwa mtu akiacha Kazi ama kuachishwa, atalipwa mafao yake na kuamua kwenda kufanya shughuli za maendeleo.

Kwa upande wake, Katibu wa Baraza la Wazee mkoani Shinyanga, Anderson Lyimo, aliipongeza serikali kwa kupanga mipango ya kuunda kamati hiyo.

Alisema hilo ni jambo jema serikali imeamua kuwathamini wazee ambao kwa miaka yote baada ya kustaafu walikuwa wakipata shida kupata mafao yao kwa wakati na kuishia kukabiliwa na ugumu wa maisha. Lyimo alisema kumekuwapo na ucheleweshaji wa malipo ya wastaafu, kwamba mstaafu hukaa zaidi ya miaka miwili akisubiri mafao.

Naye Mratibu wa Shirika la TAWALAE ambalo linatetea haki za wazee mkoani Shinyanga, Eliasenya Nnko, aliomba serikali kuwabana waajiri kupeleka michango ya wafanyakazi katika mifuko ya hifadhi.

**Imeandaliwa na Mary Geofrey, Maulid Mbaga, Beatrice Moses. Romana Mallya (Dar), Godfrey Mushi (Arusha), Renatha Msungu, Augusta Njoji (Dodoma),Elizabeth Kilindi (Njombe), Shaban Njia (Kahama), Grace Mwakalinga (Mbeya), Marco Maduhu,(Shinyanga), Restuta Damian (Bukoba).**

# Majaliwa atoa maagizo afya vijana balehe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ametoa maagizo manne ya utekelezaji wa ajenda ya taifa ya kuwekeza katika afya maendeleo kwa vijana balehe nchini (NAIA), huku akisema mimba za utotoni bado ni tatizo kubwa na kuwataka wadau kushirikiana kutokomeza.

Akizindua ajenda hiyo ya mwaka 2021/22 hadi 2024/25 jana, Majaliwa aliwataka wadau kubuni na kuandaa afua zilizofanyiwa utafiti zenye kuleta matokeo chanya katika kutokomeza mimba za utotoni.

Alisema takwimu za mimba za utotoni zinaonyesha kuwa mwaka 2020 watoto 1,135 wa shule za msingi na 5,340 wa shule za sekondari waliacha shule kwa sababu ya kupata ujauzito wakiwa shuleni.

"Hali hii haikubaliki lazima kila mmoja kwa nafasi yake aweke mikakati ya kuwawezesha watoto wa kike kumaliza masomo yao, nitoe wito kwa Watanzania kuhusika na ulinzi wa watoto wetu,"alisema Majaliwa.

Alisema serikali itahakikisha shule za sekondari hasa za kata zinakuwa na mabweni, ili kuwalinda watoto wa kike na vishawishi vitakavyokatisha ndoto yao ya elimu.

Akitoa maagizo mengine, Majaliwa alizitaka wizara za kisekta kuhakikisha zinasimamia utekelezaji wa eneo lake kikamilifu.

"Nafahamu wapo wadau wa maendeleo kutoa tamko la taasisi zao namna zitakavyoshiriki katika utekelezaji wa agenda hii kwa kuanzia katika utekelezaji wa mpango kazi wa mwaka mwaka 2021/22 ambao utaandaliwa baada ya uzinduzi wa agenda hii,"alisema Majaliwa.

Hivyo, aliagiza Wizara ya Afya ihakikishe vijana balehe watakaothibitika na maambukizi waunganishwe na huduma za tiba. Alisema idadi ya vijana balehe wenye umri wa miaka 15-19 ni zaidi ya milioni 13 sawa na asilimia 22.9 ya idadi ya watu waliopo nchini.

Alibainisha kuwa lengo la agenda hiyo ni kuwekeza katika afya na maendeleo ya vijana balehe na imeandaliwa ili kuondoa vikwazo vya vijana hao na zinapaswa kushughulikiwa kwa kipindi kifupi.

"Agenda hii itatekelezwa katika nguzo sita ambazo ni kuzuia maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi, kutokomeza mimba za utotoni, kuzuia ukatili wa kimwili, kingono na kisaikolojia, kuimarisha hali ya lishe, watoto wa kike na kiume wanabaki shuleni wakati wote, kuwajengea ujuzi na uwezo wa kuzifikia fursa mbalimbali,"alisema Majaliwa.

Alisema taarifa ya viashiria vya Virusi Vya Ukimwi iliyotolewa mwaka 2017 inaonesha kuwa kiwango cha maambukizi mapya kwa vijana hao ni asilimia 40, kati ya maambukizi hayo asilimia 80 yanatoka kwa wasichana balehe.

"Ni kosa la jinai kufanya ngono na mwanafunzi, mtu yeyote atakaye mpa ujauzito mtoto wa shule ya msingi na sekondari dhabu yake inajulikana ni miaka 30 jela,"alisisitiza Majaliwa.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema wizara hiyo itazingatia afua zilizopo kwenye mpango huo na kuahidi kuzingatia mikakati na miongozo iliyopo.

Alisema katika utekelezaji wa agenda hiyo itaanzisha mitaala itakayosaidia wanafunzi kuhitimu wakiwa na ujuzi.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alitaja mambo tisa yatakayotekelezwa na wizara katika kusukuma mbele agenda hiyo.

Naibu Waziri, Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mwanaidi Ali Khamis, alisema agenda hiyo itaanza kutekelezwa Katika mikoa 13 ya Tanzania bara ambayo viashiria visivyoridhisha vya vijana balehe katika masuala mbalimbali ikiwamo mimba za utotoni.

Mikoa hiyo ni Geita, Katavi, Mbeya, Kigoma, Lindi, Mara, Mwanza, Rukwa, Shinyanga, Simiyu, Songwe, Tanga na Tabora. Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) Tanzania, Shalini Bahuguna, aliahidi kuendelea kushirikiana na serikali katika nyanja mbalimbali ikiwamo kuwekeza katika afya na maendeleo kwa vijana balehe.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikata utepe kuzindua ajenda ya kitaifa ya kuwekeza katika afya na maendeleo ya vijana balehe, jijini Dodoma jana. Wengine (kutoka kushoto) ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, Mwakilishi wa UNICEF nchini, Shalini Bahuguna, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima na Mwakilishi wa World Vision, Nasir Mollel. **PICHA: OWM**

# Waziri, wananchi wapewa siku 90 kuondoka eneo la hifadhi

**Na Zanura Mollel,** NGORONGORO

MAMLAKA ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), imetoa notisi ya siku 30 kwa wakazi 45 kuondoka ndani ya eneo ya hifadhi akiwamo Mbunge wa Jimbo hilo, Willium Ole Nasha, na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya, Emmanuel Shanghai.

Barua iliyotiwa saini na Kamishina wa Uhifadhi, Dk. Christopher Timbuka, inasema uamuzi huo ulitokana na kikao cha kamati ya ulinzi na usalama kilichofanyika Machi 4, mwaka huu.

Dk. Timbuka alisema notisi hiyo imetolewa kwa wananchi waliotoka eneo la Jema na Oldonyo Sambu na kurudi hifadhini, hivyo kwa mamlaka aliyopewa kwa mujibu wa kifungu Cha 23(2) (a) kikisomwa pamoja na kifungu Cha 35 Cha Sheria ya Ngorongoro Sura ya 284 mwaka 1975, ametoa maelekezo ya watu hao kuondoka eneo la uhifadhi na kuwataka kubomoa nyumba zao.

"Aliyejenga nyumba ndani ya hifadhi abomoe kwa gharama zake mwenyewe," alisema Dk. Timbuka.

Aidha, alisisitiza kuwa atakayekiuka uamuzi huo ambayo pia umeazimiwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Kwa mujibu wa Dk. Timbuka, wananchi hao waliopewa notisi ni wale waliohamishwa na kupelekwa Jema ikiwa ni pamoja na kutengenezewa miundombinu yote ya msingi ikiwamo shule na zahanati.

"Orodha iliyotolewa kuna nyumba taasisi za umma kama polisi, shule na nyumba za ibada kama makanisa," alisema.

# Jela miaka 12 mauaji rafiki wa mke wake

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Morogoro imemhukumu kifungo cha miaka 12 jela, Shija Shabani (34), mkazi wa Malinyi mkoani hapa, baada ya kupatikana na hatia ya kumuua rafiki wa mke wake bila ya kukusudia.

Akitoa hukumu hiyo, Hakimu Mkazi Hussein Mushi, alisema ametoa hukumu hiyo ili iwe fundisho kwake na kwa wengine wenye tabia za kujichukulia sheria mkononi.

Awali, Wakili wa Serikali, Neema Haule, aliiomba mahakama kumpa adhabu kali mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na jamii nzima kwa sababu kuna ongezeko kubwa la vitendo vya ukatili kwa wanawake kwa sasa.

Wakili Haule aliieleza mahakama kuwa mshtakiwa alifanya mauaji hayo Machi 2, 2017 majira ya saa 2:00 usiku katika Kijiji cha Njilwa Juu, Malinyi mkoani Morogoro, chanzo kikiwa wivu wa mapenzi.

Kwa mujibu wa Wakili Haule, mshtakiwa alimuua shemeji yake aitwaye Mageth Ngwila kwa kumchoma na kisu mgongoni akiwa amelala chumbani kwake na wadogo zake wawili baada ya kuhisi kuwa anampeleka mkewe kwa wanamume.

Ilidaiwa kwamba siku ya tukio mshtakiwa alimkuta mkewe Ewada Francisco, akiwa na Sh. 5,000 lakini baada ya kumhoji alikozitoa fedha hizo, ndipo shemeji yake, ambaye ni marehemu kwa sasa, alidakia na kusema hela amempatia yeye, jambo ambalo mshtakiwa hakutaka kuliamini na kuamua kutekeleza kitendo hicho usiku.

Naye wakili upande wa utetezi, Gozbert Kitila, aliiomba mahakama kumpa adhabu ya huruma mteja wake kwa sababu ametoa ushirikiano katika upelelezi kwa kukiri kosa.

Pia alidai kwamba mteja wake amekaa mahabusu kwa miaka minne na hajawahi kukutwa na hatia ya kosa lolote huku akiwa ni baba wa familia.

**KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI**

**JESSE MUTALEMWA LUMANYISA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Suzuki-kei yenye Na. za usajili **T493 DCM** Chassis Na. **NH 22S662307,** Engine Na. **K6A3355404** kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichokaribu.

TAARIFA YA POLISI.

**MOR/MOR/RB/194673/2021.**

MAHOJIANO MAALUM:

# Waziri wa Magufuli afichua siri alivyokwepa kashfa mamilioni

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha 2019/20, mbali na mambo mengine, imeanika matumizi ya fedha katika Wizara ya Maliasili na Utalii na taasisi zilizo chini yake.

Katika ripoti hiyo iliyowasilisha bungeni wiki iliyopita, CAG Charles Kichere, anapendekeza kuchukuliwa hatua kwa baadhi ya vigogo wa wizara hiyo, wakiwamo maofisa masuhuli huku aliyekuwa waziri wake, Dk. Hamis Kigwangalla, akitajwa kuhusika katika baadhi ya dosari za matumizi ya fedha zilizobainika.

Mbunge wa Geita Mjini, Constantine Kanyasu (CCM) (pichani), alikuwa Naibu Waziri wakati matumizi hayo ya fedha yakifanyika wizarani huko, lakini jina lake halimo kwenye orodha ya waliopendekezwa na CAG kuchukuliwa hatua.

Nipashe imezungumza na Kanyasu kwenye jiji la Dodoma kwa lengo la kufahamu siri ya kutoingia kwenye kashfa hiyo pamoja na mambo mengine muhimu ya kitaifa. Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na mbunge huyo;-

**SWALI: Ripoti ya CAG imebainisha kuwapo kwa matumizi mabaya fedha kwenye Wizara ya Maliasili na Utalii. Nini siri ya jina lako kutokuwa sehemu ya wakitajwa na CAG ilhali ulikuwa Naibu Waziri?**

**JIBU:** Ni kweli nilikuwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa miaka miwili na nusu. Kilichoripotiwa na CAG siyo wizi moja kwa moja, bali kukiukwa kwa taratibu za matumizi ya fedha. Huenda fedha zimetumika kihalali lakini utaratibu uliotumika ndiyo shida. Watu wanachanganya habari ya huyu ni mwizi na huyu amekiuka taratibu za matumizi ya fedha.

Kwa nini mimi siwezi kutajwa? Ni kwa sababu katika matukio yote haya ambayo inaonekana Mheshimiwa Waziri alishiriki, mimi sikuwa sehemu yake. Alikuwa anaandaa hayo matamasha kwa kushirikiana na wadau wa utalii mimi nikiwa ninaendelea na programu zingine.

Lakini jambo lingine la kuzingatiwa ni kwamba mwenye 'vote' ni waziri, naibu waziri hana 'vote', naibu waziri ni waziri kama waziri hayupo, lakini akiwapo waziri, mwenye 'vote' ni waziri na mtendaji mkuu ni Katibu Mkuu wa Wizara.

Hata Naibu Katibu Mkuu hawezi kutuhumiwa katika jambo hilo, vinginevyo awe aliachiwa ofisi akatia saini. Ndiyo maana huwezi kumwona Naibu Waziri katika maeneo hayo.



Lakini jambo lingine, mimi siku zote, nimekuwa mtumishi wa umma kwa muda mrefu nikiwa DC (Mkuu wa Wilaya), ninaheshimu sana fedha za serikali, za walipakodi. Huwezi kunishirikisha kwa namna yoyoye ile kufanya mpango wa kujaribu kubadili matumizi ya fedha za serikali. Kwa hiyo, inawezakana hilo limeniokoa.

**SWALI: Ni jambo gani moja tu utamkumbuka Hayati Rais John Magufuli?**

**JIBU:** JPM amenifundisha uongozi. Rais Magufuli alikuwa anafikiria sana, anakufuatilia mambo yake anapokuagiza na kuheshimu sana anapokupa nafasi. Mara nyingi aliponituma kazi na alinipongeza na kuniambia 'ongeza bidii'.

Kwa kweli, Rais Magufuli alikuwa anafanya kazi kwa bidii kubwa sana. Nitamkumbuka kwa namna ambavyo amenisaidia kukuza uwezo wangu wa kiuongozi.

**SWALI: Ukipata nafasi ya kuzungumza na Rais Samia Suluhu Hassan leo kwa dakika moja, utamshauri jambo gani muhimu kwa taifa?**

**JIBU:** Kama mwanasiasa, nitamshauri awe Rais wa watu wote, awasikilize wote. Wako watakaompinga, wapo watakaomuunga mkono, wako watakaomkosoa, watakaomwona anafanya jambo jema.

Sasa, ni kupitia humo anaweza kujua marafiki wabaya na marafiki wazuri. Kwa hiyo, hilo ndo jambo ambalo ninaweza kumshauri Mheshimiwa Rais awasikilize wote.

**SWALI: Nini shida kuu ya Jimbo la Geita Mjini kwa sasa?**

**JIBU:** Geita ni makao makuu ya mkoa. Shida kuu kwa sasa ni miundombinu inayoendana na hadhi ya mkoa. Bado barabara zetu zina hadhi ya kiwilaya wilaya hivi. Pale mjini sasa tunajenga barabara za lami. Bado tuna shida hiyo ya miundombinu.

Shida nyingine ni maji. Mji unakua kwa kasi sana lakini maji yaliyopo yanatosha halmashauri ya mji. Kwa hiyo, tunapambana kupata maji ya kutosha. Vitu vingine vyote viko kwenye 'control'.

**SWALI: Marekebisho ya Sheria ya Madini yameleta manufaa yapi kwa Mji wa Geita?**

**JIBU:** Kabla Mheshimiwa Dk. Magufuli hajaingia madarakani, kulikuwa na uhasama mkubwa kati ya wananchi na wawekezaji wakubwa wa madini. Ni kwa sababu wawekezaji walikuwa wanachimba na kuacha mashimo.

Mabadiliko ya sheria yaliwapa wananchi nafasi ya kunufaika na rasilimali za nchi. Kumeanzishwa masoko ya dhahabu, yale masoko yameongeza mapato ya halmashauri na yameboresha kipato cha wananchi.

Kwa hiyo, mabadiliko ya sheria yameifanya halmashauri kukusanya mapato mengi zaidi kutokana na mgodi.

Sheria ile ilileta mabadiliko makubwa kwenye migodi kuwajabika kwa jamii. Tumejenga zahanati 24, tumejenga shule 25 kwa mapato hayo ya ndani, tumejenga soko na tumejenga barabara.

Kwa hiyo, mabadiliko haya ya sheria yameleta mabadiliko na manufaa makubwa sana kwa sababu wananchi wa Geita kwa miaka 20 walikuwa hajawahi kuona faida ya madini.

Tatizo lililopo sasa kwenye utekelezaji wa ile sheria lipo katika 'local content'. Utekelezaji wa ile sheria haujasimamiwa vizuri kwa maana uagizaji wa malighafi kutoka nje kwa ajili ya migodi hauzingati ile sheria.

Waziri alisimamie vizuri eneo hili kwa sababu wakinunua waagizaji wa ndani, serikali itapata kodi stahiki kuliko kuruhusu kampuni zijiagizie zenyewe mzigo kutoka nje.



HABARI KITAIFA

## Waomba elimu zaidi ugonjwa wa 'himofilia'

**Na Romana Mallya**

WAZAZI na walezi wa watoto wenye matatizo ya ugonjwa wa himofilia wameiomba serikali kutoa elimu zaidi kwa wataalam wa afya kuanzia ngazi za chini za huduma ili badala ya kwenda Muhimbili waishie huko kupata matibabu.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) kwa niaba ya wazazi wenye watoto wa himofilia, Regina Shirima, alisema moja ya matatizo wanayokumbana nayo ni wahudumu kutoufahamu ugonjwa huo wanapowapeleka watoto kupata huduma.

Jana, ilikuwa siku ya maadhimisho ya ugonjwa huo ambao kitaalam ni ukosefu wa chembechembe za protini zinazosaidia damu kuganda mwilini.

Alisema asilimia kubwa ya wahudumu wa afya hawaufahamu ugonjwa huo hivyo wanapowapeleka watoto wao ili waweze kupata huduma ya dawa maalum (factors), wamekuwa hawaelewi.

"Hospitali za chini hawajui ugonjwa huu, serikali itusaidie itoe elimu kwa wahudumu wa afya, ili tunapowapeleka watoto kwa ajili ya kuchomwa dawa maalum wawe na uelewa nao," alisema.

Pia waliiomba serikali iwasaidie ugonjwa huo uingie kwenye masomo ya mashuleni ili wanafunzi waufahamu kama wanavyosoma magonjwa mengine.

Mwanzilishi wa Chama cha Himofilia Tanzania, Abdulsadiki Muhina, alielezea alivyopitia hatua mbalimbali za ugonjwa huo tangu akiwa mdogo hadi wakati huu ikiwa ni pamoja ajali aliyopata lakini ameendelea kusimama na kufanya kazi na kuwa baba wa watoto wawili wa familia yake. "Mungu amenipa hili ninajua ana kusudi lake halijanikatisha tamaa, ninafanya kazi isiyotumia nguvu na nina watoto wawili, tukifuata masharti tutafika mbali," aliwatia moyo wazazi wenye watoto wa himofilia.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, alisema maisha ya watu hao yanahitaji uangalizi mkubwa ili kuzuia uvujaji damu, ulemavu na vifo.

"Hulazimika kupimwa ili kubaini aina ya himofilia inayomsumbua na kupata matibabu ya kuchomwa factor (chembechembe za protini zilizokosekana mwilini) ili kusaidia kugandisha damu, matibabu yake ni ghali na upatikanaji wake ni mgumu," alisema. Alisema takwimu za duniani zinaonyesha mtu mmoja kati ya 10,000 ana tatizo hilo na kwa Tanzania inakadiriwa kuna wagonjwa wapatao 6,000 hadi 12,000.

"Takwimu zinaonyesha asilimia 97 ya watu wenye ugonjwa huu duniani bado hawajagundulika ambapo kwa Tanzania waliotambulika na wanaendelea na matibabu ni 167 tu," alisema. Alisema Novemba 20, mwaka jana, Muhimbili kwa kushirikiana na wadau wa afya Novo Nordisk Foundation (NNF) na Novo Nordisk Hemophilia Foundatin (MMHF), ilianzisha kazi ya upatikanaji wa huduma unaotekelezwa kati ya Tanzania na Kenya.

Alisema lengo ni kuunga mkono jitihada za serikali kupitia wizara ya afya katika kupunguza madhara na vifo vinavyotokana na ugonjwa huo.




Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martin Shigella (kushoto), akikabidhi mfano wa ufunguo wa Bajaji kwa mlemavu wa viungo, Seleman Zuberi wa kituo cha watoto na vijana wenye ulemavu cha YDCP, wakati Taasisi ya Islamic Help Tanzania, ilipotoa msaada wa Bajaji tano, pikipiki tatu na mifugo aina ya mbuzi 740 kwa kituo hicho, jijini Tanga juzi. Wa (pili kulia) ni Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Amjad Khan na (kulia) ni Mratibu wa kituo hicho, Leopord Abeid. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Aweso atoa maagizo kwa wakurugenzi wa maji

**Na Paul Mabaja,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Juma Aweso, amewataka wakurungenzi wa mamlaka za maji nchini, kuhakikisha wanaweka mikakati ya kupunguza upotevu wa maji, ambao umekuwa ukichangia kupotea kwa mapato kila mwezi Sh. bilioni 9.5.

Aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati akizindua Kampeni ya Kudhibiti Upotevu wa Maji nchini inayoratibiwa na Jumuiya ya Umoja wa Wasambazi Maji (ATAWAS).

Alisema upotevu wa maji nchini katika mamlaka mbalimbali za maji imekuwa kero ambayo inasababisha kiasi kikubwa cha mapato kupotea.

Alisema kutokana na hali hiyo wakurugenzi pamoja na wadau mbalimbali katika sekta ya maji wanatakiwa kuhakikisha wanakuwa na mikakati ya kudhibiti upotevu huo wa maji.

"Wakurugenzi wangu naomba mjipange kama msipojipanga mimi pamoja na wasaidizi wangu tutahakikisha tunawapanga wenyewe, kama yalivyo maagizo ya Rais Mama Samia iwe jua iwe mvua lazima wananchi wetu wapate huduma ya majini,"alisema Aweso.

Vilevile, alisema kiasi cha maji ambacho kimekuwa kikipotea kila siku ni kikubwa ambacho hakitakiwi kuendelea kuvumiliwa bali hatua za haraka zichukuliwe ili kukabilina na tatizo hilo.

"Takribani asilimia 36 ya maji yanapotea kila mwezi lakini pia kiasi cha fedha takribani sh. bilioni 9.5 zinapotea kila mwezi ambazo tungeweza kuzifanyia mambo mengine ya maendeleo,"alisema Aweso.

Alisema kuwa njia ambazo zimekuwa zikichangia kupotea kwa maji ni pamoja na watu kujiunganisha huduma hiyo kinyume na utaratibu.

Alisema njia nyingine ni ubovu wa miundombinu ya maji ambayo imekuwa ikichukua muda mrefu kufanyiwa ukarabati na mamlaka husika.

Aidha, Aweso aliwataka wananchi kuwa walinzi wa miradi ya maji ambayo serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha ili idumu na kutoa huduma kwa muda mrefu kwa wananchi.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Antony Sanga, alisema kuwa tatizo la upotevu wa maji nchini bado kubwa hali ambayo wao peke yao hawawezi kuikomesha bila ya kushirikisha wadau wengine.

Kadhalika, alisema tatizo lingine katika upotevu wa maji lipo katika mita zinazotumika na mamlaka za maji kutokuwa na ubora, hivyo ipo haja kufanyika kwa utafiti ili kupata zilizo bora.

Mwenyekiti wa Bodi ya ATAWAS, Mhandisi Geofrey Hilly alisema kuwa lengo la kampeni hiyo ni kudhibiti upotevu wa maji katika maeneo mbalimbali nchini na kuongeza mapato.

"Katika Kampeni hii tutatumia makundi mbalimbali wakiwamo watu wa Media ili kufikisha ujumbe kwani wanaohusika katika upotevu wa huduma hii ni watu ambao wapo katika mazingira hayohayo,"alisema Hilly.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa Benki ya Equity, Esther Kitoke, ambayo ni moja ya wadau wa kampeni hiyo alisema wameshiriki katika kuanzisha huduma ya mkopo kwa wananchi kwa ajili ya kuunganishiwa huduma za maji.

Kitoke, alisema moja kati ya sababu za upotevu wa maji ni idadi kubwa ya watu kutokuwa na huduma hiyo, hivyo watu kutumia njia zisizo rasmi kupata huduma hiyo muhimu.

## Mchumi kortini tuhuma za kusababishia hasara serikali

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Singida, imempandisha kizimbani Mchumi wa Mkoa wa Mbeya, Halima Mpita, kwa tuhuma za kusababishia serikali hasara ya Sh.milioni 33.1 kwa kufanya malipo ya mbao hewa kwenye shule za sekondari katika Wilaya ya Iramba.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Singida, Adili Elinipenda, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa ya Januari hadi Machi.

Elinipenda alisema taasisi hiyo ni chombo chenye kusimamia mapambano dhidi ya rushwa nchini ikiongozwa na sheria ya TAKUKURU namba 11 ya mwaka 2007.

Katika hatua nyingine, Elinipenda alisema taasisi hiyo iliwafikisha mahakamani, Simion Shango na Joseph Shani kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa ya Sh. milioni 1.025. Kwa mujibu wa Elinipenda katika kesi ya jinai namba 4 ya mwaka 2020 ilimhusu Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kinyarimi, wilayani Ikungi, John Mbua, aliyekuwa akikabiliwa na tuhuma za kushawishi rushwa ya Sh. 150,000 na kupokea Sh.100,000 ili amsaidie fundi aliyekuwa na madai ili alipwe. Hata hivyo kwa mujibu wa Elinipenda katika hukumu yake iliyotolewa na mahakama hiyo, mshitakiwa huyo alihukumiwa adhabu ya kulipa faini ya Sh. 500,000 au kwenda kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka mitatu jela.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kamati kutathmini kikokotoo mafao izingatie ya watumishi

**HATIMAYE** serikali imetangaza kuwa imeunda kamati mahsusi kwa ajili ya kutathmini dosari zilizojitokeza katika kanuni mpya za ulipaji mafao, maarufu kama kikokotoo ya watumishi baada ya kustaafu.

Mkanganyiko huo unatokana na kanuni hiyo kulalamikiwa na wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa vyama vya wafanyakazi, wasomi na wafanyakazi wenyewe baada ya kupitishwa na Bunge la Tanzania mwaka 2017.

Katika kanuni hiyo, ilibainishwa kwamba mfanyakazi ambaye ni mwanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Wafanyakazi wa Sekta Binafsi (NSSF), wakati wa kustaafu, atalipwa kwa mkupuo asilimia 25 ya michango yake na asilimia 75 iliyobaki atalipwa kama mshahara kwa miaka 12.5.

Kwa mantiki hiyo, kama mfanyakazi huyo michango yake katika mfuko huo ni Sh. milioni 80, malipo yake ya mkupuo yatakuwa Sh. milioni 20, hivyo kiasi kilichobaki (Sh. milioni 60) atalipwa kila mwezi kama mshahara kwa kipindi kilichotajwa. Hapo ndipo mgogoro ulipoanza kutokana na ukweli kwamba kiasi kikubwa cha fedha kinabaki kwenye mfuko.

Ni bayana kwamba kwa kanuni hiyo, mfanyakazi badala ya kufurahia jasho la utumishi wake anaingia kwenye mateso na majuto kwani muda uliobaki ataishi kwa kusikitika tu. Hatua hiyo pia inaweza kusababisha baadhi ya wastaafu kupatwa na maradhi kama sonona, msongo wa mawazo, kiharusi na hata kupoteza maisha.

Kutokana na ukweli huo, ndiyo maana aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli, aliingilia kati na kutaka utekelezaji wa sheria hiyo usimamishwe na wahusika kutafakari upya huku akiagiza mchakato wa kanuni hiyo uanze kutekelewa mwaka 2023.

Dk. Magufuli kakuishia hapo bali alitengua hata uteuzi wa aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa iliyokuwa Mamlaka ya Usimamizi na Udhibiti wa Sekta ya Hifadhi ya Jamii (SSRA), Irene Isaka.

Kuundwa kwa kamati hiyo maalum, kumeamsha matumaini mapya kwa wafanyakazi kwamba huenda wakafikiriwa upya na kwamba badala ya kuumizwa, kama ilivyokuwa katika kanuni iliyopitishwa, sasa watafurahia matunda ya utumishi wao. Wadau mbalimbali wametoa maoni yao huku wengi wakionyesha matumaini juu ya jambo hilo.


Ni rai yetu kwamba kamati hiyo, katika kutathmini dosari hizo, itumie busara zaidi kwa kutambua kwamba wanufaika wa mafao hayo wametumika kwa moyo wao wote, hivyo wanapaswa kunufaika na jasho lao badala ya kuwa mateso katika maisha yao yaliyobaki.

Kama alivyosema Waziri Mkuu Bungeni Jumanne wiki hii, ni imani kwamba kamati hiyo itazingatia maagizo ya Rais aliyoyatoa ili kupata kanuni nzuri na bora itakayokidhi matarajio ya wafanyakazi.

Haiingii akilini kuona kwamba mfanyakazi aliyetoa mchango wake kwa maendeleo ya taifa, ama katika sekta ya umma au binafsi, akipata mafao kiduchu na mamilioni ya fedha zake yakiendelea kushikiliwa na mfuko husika wa hifadhi ya jamii.

Ni vyema mfanyakazi huyu akapewa fedha zake hata kama ni asilimia 70 ili akanufaike nazo huku kiasi kidogo kilichobaki kwenye mfuko, akalipwa kila mwezi kama kifuta jasho chake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kumbe kuwatetea madereva wa 'bodaboda' inataka moyo

Na Sabato Kasika

**KAZI** ya kuendesha pikipiki za abiria, maarufu kama bodaboda, imerahisisha usafiri kwa kiasi fulani na pia imeajiri vijana wengi na baadhi yao imewapunguzia ukali wa maisha na pia kuachana na vitendo vya uhalifu.

pamoja na kuwapo kwa fursa hiyo ya ajira, kumekuwapo na mtindo wa kutotii sheria unaofanywa na baadhi yao na hata wakati mwingine kusababisha ajali ambazo kama wangekuwa makini wangeweza kuziepuka.

Madereva wa bodaboda, wamekuwa wakitajwa kuwa wanaongoza kwa kuvunja sheria za barabarani na kusababisha ajali za makusudi, ambazo wakati mwingine hugharimu maisha yao, ya abiria au ya waenda kwa miguu.

Ajira yao kwa upande mwingine, imegeuka kuwa balaa, kutokana na baadhi yao kutozingatia sheria za barabarani na kusababisha ajali za mara kwa mara, ambazo pia huwaacha ulemavu wa kudumu, kwa makosa yao.

Miongoni mwa makosa wanayodaiwa kuyafanya ni kupita magari bila tahadhari, kutovaa kofia ngumu (helmet) na kuvuka kwenye makutano ya barabara kabla hawajaruhusiwa na taa za kuongozea magari.

Mazoea hayo ya baadhi yao kuvuka makutano ya barabara bila kuruhusiwa na taa, wanapokosea hesabu, hujikuta wakigongwa na magari na kupoteza maisha, kupata ulemavu wa kudumu au majeraha.

Mwendelezo wa kutotii sheria bila shuruti, hasa kwa madereva wa jijini Dar es Salaam upo pia kwenye barabara za mabasi ya mwendokasi, ambazo ni maelekezo ni kwamba, zitumike kwa mabasi hayo tu.

Lakini madereva wa bodaboda wamekuwa mstari wa mbele kupita kwenye barabara hizo kana kwamba hawajui kuwa ni makosa, hali ambayo ni hatari kwa usalama wao na wa abiria pia. Wakazi wa jijini Dar es Salaam, watakuwa wanakumbuka kuwa mara tu baada ya mabasi ya mwendokasi kuanza kusafirisha abiria, baadhi ya madereva wa 'bodaboda' waligongwa na mabasi.

Baadaye serikali alipiga marufuku, magari binafsi, umma na 'bodaboda' kupita kwenye barabara hizo, lakini marufuku hiyo ni kama haikuwaingia akilini baadhi ya madereva wa bodaboda na huenda wanahitaji kushurutishwa.

Kwa ujumla ni kwamba, ajali za bodaboda', zimepoteza maisha ya wengi, kusababisha watoto kuwa yatima, hali iliyosababisha serikali kuweka faini kubwa ili kuwafanya wawe makini wanapoendesha vyombo hivyo vya moto.

Faini ambayo waendesha 'bodaboda' wanatozwa wanapokiuka sheria za usalama barabarani ni Sh. 30,000 kama ambavyo ilivyo kwa dereva anaendesha gari linalobeba abiria zaidi ya 30.

Hata hivyo, wiki iliyopita, mbunge wa Musoma Mjini mkoani Mara, Vedastus Mathayo, alijaribu kuwatetea bungeni akitaka wapunguziwe faini hiyo, kwa madai kwamba, kiasi hicho ni kikubwa kinawaumiza.

Akijenga hoja, alisema, hiyo ndiyo ajira yao, hivyo kuwatoza faini ya Sh. 30,000 kama ilivyo kwa madereva wa mabasi ni sawa na kuwaumiza, kwa madai kwamba, wao wanabeba abiria mmoja.

Mathayo alisema, kuendelea kuwatoza faini hiyo, itakuwa ni sawa na kuwaumiza na kuhatarisha ajira yao hiyo ambayo wanaitegemea kuendesha maisha yao ya kila siku na familia zao.

Kutokana na hoja yake hiyo, Naibu Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Khamis Hamza Chilo, alimkumbusha kuwa hadi Desemba mwaka jana, bodaboda zilikuwa zimesababisha ajali 164, vifo 134 na majeruhi 129.

Akaweka wazi kuwa serikali bado haijaona umuhimu wa kuwapunguzia faini hiyo, ambayo ililenga kuwafanya madereva wa 'bodaboda' wajifunze kuheshimu sheria za barabarani ili kupunguza ajali.

Lakini kwa kuwa bado wanaendelea kusababisha ajali, serikali haiwezi kupunguza kiwango cha faini hiyo ambacho kiliwekwa ili kuwafanya wabadilike na kufanya kazi kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Kwa takwimu hizo za naibu waziri na maelezo yake, ni wazi kwamba kuwatetea madereva 'bodaboda' inataka moyo, kutokana na ukweli kwamba, kuwapo kwa sheria za usalama barabarani, bado hawazizingatii.

Vitendo ambavyo baadhi yao hufanya barabarani, huwa vinaashiria kwamba, wamezoea kutii sheria kwa shuruti, hivyo si vibaya kuendelea kuwapo kwa adhabu hiyo ili hatimaye wote waweze kubadilika.

SAFU

AFYA

# Kula pera kwa faida hizi kiafya

Na Mwandishi Wetu

PERA ni moja ya matunda yanayopatikana maeneo mengi duniani na limekuwa maarufu kwa milo katika namna tofauti. Linaweza kuliwa kama tunda likiwa limeiva lakini pia linatumika kutengenezea sharubati (juisi) likiwa lenyewe au kwa kuchanganywa na matunda mengine.

Tunda hili ni kati ya matunda yenye kutia afya zaidi katika miili yetu hasa kwa wale wenye maradhi sugu. Inaelezwa kuwa hata wazee wa zamani, walikuwa wakitumia mmea huu kwa ajili ya tiba asili.

Pamoja na kutumiwa mara kwa mara na watu, wengi hawajui kama lina faida mbalimbali katika afya ya mwili.

Moja ya faida za pera ni kwamba hushusha kiwango cha sukari kwenye damu. Licha ya kwamba lina utamu, ni moja ya matunda ambayo ni mujarabu kwa kushusha kiwango cha sukari. Hii ni habari njema kwa wenye kisukari na wale wenye tatizo la homoni ya insulin.

Hapa tunazungumzia majani ya mpera ni si tunda lenyewe. Katika utafiti waliofanyiwa watu 19, imethibitisha kuwa kunywa majimaji yatokanayo na majani ya mpera husaidia kushusha kiwango cha sukari.

Utafiti mwingine waliofanyiwa watu 20 wenye aina ya kisukari aina ya pili (type 2 diabetes) iligundulika kwamba kunywa maji yaliyochemshwa kutokana na majani ya mpera, yanashusha sukari kwa asilimia 10.

### AFYA YA MOYO

Mbali na kusaidia kushusha sukari mwilini, pera husaidia katika kuimarisha na kulinda afya ya moyo. Wataalamu wa afya wanabainisha kwamba pera lina vitamini nyingi pamoja na vidhibiti sumu (antioxidant) ambazo husaidia katika kulinda moyo dhidi ya mionzi na hatari zingine.

Pia inaelezwa kwamba pera lina kiwango kikubwa cha madini ya potassium (chumvi) pamoja na kambakamba ambazo husaidia katika kuimarisha afya ya moyo.

Pia ulaji wa mapera unaelezwa kuwa husaidia kuondoa lehemu (cholesterol) mwilini, hivyo kupunguza nafasi ya kupata maradhi ya shinikizo la damu la juu (HBP) pamoja na uwezekano wa kupata kiharusi (stroke).

### MAUMIVU YA TUMBO

Pera pia husaidia kupunguza maumivu ya tumbo la chango kwa wanawake. Wanawake wengi wanapata maumivu makali wakati wa hedhi, hivyo wanashauriwa kuutumia maji ya majani ya pera ili kuzuia tatizo hilo.

Utafiti unaonyesha kwamba wanawake 197 ambao hupata maumivu wakati wa hedhi walionyesha kupata nafuu baada ya kunywa maji ya mpera.

Kwa mujibu wa utafiti huo, miligram sita za maji ya majani ya mpera husaidia kupunguza maumivu haya. Pia utafiti zaidi umeonyesha kuwa majani ya mpera husaidia kupunguza maumivu hayo maradufu tofauti na kutumia dawa za kupunguza maumivu.

Pia utafiti unaonesha kuwa majani ya mpera hupunguza maumivu wakati wa kutoa haja ndogo kwa wale wanaopata maumivu haya.

### MMENG'ENYO WA CHAKULA

Kwa wale wenye tatizo la mmeng'enyo wa chakula, habari njema ni kwamba pera ni kati ya matunda yenye kambakamba ambazo kitaalamu hujulikana kama 'fibre' ambazo husaidia katika kuboresha mchakato wa kukimeng'enya chakula.



Kutokana na umuhimu huo, pera husaidia tatizo la kutokupata choo. Pia utafiti unaonyesha kwamba pera moja hukusanya asilimia 12 ya kambakamba zinazohitajika mwilini kwa siku.

Pia majani ya pera yakitengenezwa, majimaji yake husaidia katika kuboresha afya ya mfumo mzima wa mmeng'enyo wa chakula.

Aidha, Kwa wale wenye tatizo la kuharisha, majani ya mpera ni mujarabu sana katika kuondoa au kupunguza tatizo. Pia utafiti zaidi unaonyesha kuwa pera husaidia katika kuua vijidudu vibaya ndani ya tumbo.

### KUPUNGUZA UZITO

Wataalamu wa afya wanabainisha kuwa pera husaidia katika kupunguza uzito. Inaelezwa kuwa pera lina 'calory' chache na lina 'fiber' nyingi ambazo kwa pamoja husaidia kumfanya mtu ahisi kushiba mapema, hivyo kumpunguzia kula sana. Hali hii husaidia katika kupunguza uzito mwili.

### KUDHIBITI SARATANI

Pera linaelezwa kuwa husaidia kulinda mwili dhidi ya maradhi ya saratani. Utafiti unaonyesha kuwa pera lina 'anticancer effect' ambazo husaidia mwili kuzuia uwezekano wa kupata maradhi ya saratani. Pia husaidia kuuwa seli za saratani ndani ya mwili wa binadamu.

Aidha pera ni moja ya matunda yenye vitamini C nyingi ambazo husaidia kuupa nguvu mwili katika kupambana na maradhi.

### AFYA YA NGOZI

Kwa afya njema ya ngozi, pera ni mujarabu katika kuhakikisha inabaki salama muda wote. Pera husaidia kuondoa mikunjo kwenye ngozi na kuua baadhi ya bakteria kwenye ngozi.

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kumsema Magufuli isiwe tija au nongwa



Na Joseph Kulangwa

**Hii iliyompenda sana ina watu waliojitokeza na kuwatisha wale wa kambi nyingine, kuwa kama haitaacha kumsema vibaya marehemu, kitakachowakumba shauri yao.**

KIFO ni tukio la kusikitisha, lakini ni sehemu ya uumbaji wa Mungu, kwamba kila kiumbe hai huishi lakini hatimaye hukumbwa na kifo na kufariki dunia. Tukio hilo husababisha majonzi na simanzi katika jamii, husuan kwa wafiwa.

Kiongozi wa familia anapokuwa amekumbwa na mauti na kufariki dunia, huacha simanzi kubwa kwa wategemezi, ndugu na jamaa na hasa aliokuwa nao karibu, wakimtegemea kwa kila jambo.

Lakini kifo hufuatiwa na msiba au maombolezo yaliyogubikwa maneno maneno, mazuri na hata mabaya, kumhusu marehemu au hata jamii iliyobaki, kwa maana ya wafiwa, ili mradi halikosekani la kusemwa.

Hivi karibuni, Watanzania walifiwa na kiongozi wao mkuu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk John Magufuli, baada ya kuugua na hatimaye aliyemtoa akamtwaa na jina lake likahimidiwa kama ilivyo ada.

Mara tu baada ya kutokea kifo hicho, kutokana na Katiba ya nchi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Samia Suluhu Hassan akaapishwa kuwa Rais wa sita, lakini majonzi na maombolezo, vikaendelea hadi kuhitimika.

Siku za karibuni, Watanzania baadhi yao, wakaona haitoshi, baada ya kupambana na ugonjwa wa Uviko-19 ambao bado upo, wakaona ni bora wajizushie ugonjwa mwingine uwashughulishe, hauna dawa ya hospitali wala ya waganga wa kienyejimaneno na malumbano.

Ugonjwa huu umekuwapo kwa Watanzania hasa kila linapotokea jambo na kuendelea nao, mpaka wanapoona sasa basi, lakini wameshatoana jasho na hata machozi, kusemasema hili na lile, kumsema huyu na yule, ilimradi basi tu.

Hivi sasa kumetokea kusemana, kuna kambi mbili zisizo rasmi, moja ni ile inayodhani na kujiaminisha, kuwa ilimpenda sana Rais Magufuli, lakini ipo nyingine ambayo inajinasibu kutompenda Rais Magufuli. Na kila kambi ina sababu zake.

Hii iliyompenda sana ina watu waliojitokeza na kuwatisha wale wa kambi nyingine, kuwa kama haitaacha kumsema vibaya marehemu, kitakachowakumba shauri yao. Inasema kama tabia hii haitakoma, hakutakuwa na utulivu na amani nchini.

Ile ya pili inatamba kuwa ni wakati wake sasa kusema, kwa sababu wakati wa uhai wa Rais Magufuli ilifungwa sana midomo ikakosa pa kusemea, hata pale ilipokuwa ikitaka iseme kilichokuwa kikiisibu. Na kambi hiyo inasema inachokiona kuwa ni mabaya ya Magufuli.

Kambi zote zina haki ya kutoa hadharani hisia zao, ili mradi hazivunji sheria ya nchi kwa kuhakikisha usalama, utulivu na amani vinadumu nchini. Bila shaka kauli tu na hisia, haviwezi kujeruhi mtu kiasi cha kumwaga damu, eti kwa sababu Rais wa tano amesemwa.

Hakuna ubishi, kwamba Rais Magufuli akiwa madarakani alifanya aliyoyafanya kwa uwezo wake wote, katika kulileteа Taifa maendeleo. Kuna makubwa aliyoyafanya na yanaonekana. Lakini ni uamuzi wa kila mmoja kuyaona na kuyatambua au kutoyatambua, lakini yapo.

Hakuna kiumbe wa Mungu mwenye kinga asili ya kusemwa vibaya au vizuri, yote hayo ni mapenzi ya Mungu, ndiyo sababu Mungu huyo huyo akamuumba shetani na mpaka sasa hajamuua na yuko kazini, upande huu Mungu, upande ule yeye.

Watanzania wanaovutana katika pande hizo mbili, wamefikia hatua ya kutukanana na hata kudhalilishana, wengine wakizuia hata kubeza fikra za kitaalamu zinazotolewa dhidi ya mradi au jambo fulani, kwa kuwa tu liliasisiwa na JPM.

Wengine wanafikia hatua ya kuwaona wanaomtetea JPM, kama makatili waliohusika na machungu yaliyowapata ndugu zao wakati wa utawala wa kiongozi huyo, tena wakihanikiza kuwa uongozi ulikuwa wa mtu mmoja, na si wa Serikali kiujumla!

Tusimkwaze Rais Samia, tuachane na malumbano, tupeane nafasi kila aliye na lake aliseme kwa uhuru, lakini lisiwe la kupakazia au kuzushia mtu ambaye ametangulia mbele za haki, lakini kama ni la kweli basi lisemwe tu, tujifunze. Wengi waliotangulia walisemwa na wanasemwa mbona hakuna tatizo?

## KONA YA UKWELI

# Viongozi vigeugeu ni hatari kwa taifa



Na Thobias Mwanakatwe

**Alianza aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kingwangalla, kwa kutoa ushauri kuwa mashine za kujifukiza zilizofungwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) zilizotengenezwa na SIDO ili kusaidia wagonjwa kupata tiba ya mfumo wa upumuaji kwa kutumia dawa za tiba asili hazifai, hivyo zifungwe!**

TANGU kutokea kifo cha aliyekuwa rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli Machi 17, mwaka huu, mijadala kemkem imeibuka kwenye mitandao yenye umuhimu mkubwa kwa mustakabali wa taifa letu.

Kwanza, wako watu waliofurahia kifo cha Rais Dk. Magufuli wakidhani kuwa serikali mpya ya Rais Samia Suluhu Hassan imeingia kupindua 'legacy' ya Dk. Magufuli ya kusimamia maslahi ya Watanzania, hususani wanyonge.

Pia wako baadhi ya watu ambao sasa wanawabeza na kuwatukana wale waliokuwa wakiunga mkono juhudi za kiukombozi za Dk. Magufuli ambazo Rais wa sasa alikuwa sehemu yake. Wako pia watu ambao kwa akili zao wanadhani kuwa tatizo kubwa la Tanzania lilikuwa Dk. Magufuli aliyejitoa sadaka kupambana na ubeberu ili kulinda maslahi mapana ya Tanzania.

Kingine ni kwamba kuna watu wanataka 'kumwelekeza' Rais Samia afanye wanavyotaka kukidhi maslahi yao binafsi na wengine wamekuwa wakitetea maslahi yao binafsi na ya mabeberu waziwazi wakati Magufuli alijitoa muhanga kutetea maslahi ya Watanzania na Waafrika walionyonywa na kukandamizwa kwa miaka mingi.

Kitu cha msingi cha kujiuliza je, tunapaswa kutumia sera gani kuhakikisha Waafrika tunaondokana na unyonge huu wa karne nyingi ambao unaendekezwa na kuendelezwa na wale wale waliojenga mifumo yote, ikiwamo ya siasa, kijamii na kiuchumi, ili hatimaye tujitawale na kujitegemea kwa kutumia rasilmali zetu?

Kibaya zaidi ambacho ndicho nakijadili leo ni wimbi lililoanza kujitokeza la viongozi wengine waliokuwa na nyadhifa mbalimbali awamu ya tano kuanza kushambulia na kupinga hadharani mambo yaliyokuwa yakifanywa na Dk. Magufuli.

Hawa viongozi vinyonga, kipindi cha utawala wa JPM walikuwa na rangi nyingine na sasa utawala wa Mama Samia wamejigeuza na kujionyesha rangi nyingine. Hakika viongozi wa aina hii ni hatari kwa taifa.

Alianza aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kingwangalla, kwa kutoa ushauri kuwa mashine za kujifukiza zilizofungwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) zilizotengenezwa na SIDO ili kusaidia wagonjwa kupata tiba ya mfumo wa upumuaji kwa kutumia dawa za tiba asili hazifai, hivyo zifungwe!

Tamko la Dk. Kingwangalla lilishutumiwa sana kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa kuwa kiongozi kinyonga kwa kuwa enzi za utawala wa JPM, alikuwa mpigadebe mzuri wa kutumia njia hiyo ya kujifukiza ili kujikinga na COVID-19.

Wakati mashambulizi dhidi ya Dk. Kingwangala yakiendelea, naye Spika wa Bunge la Tanzania, Job Ndugai, akaibua suala la ujenzi wa bandari ya Bagamoyo. Ndugai ambaye alikuwa akizungumza bungeni alisema serikali iangalie upya mradi huo iwapo ni jambo jema waendelee nao kwa madai kuwa Rais (kipindi hicho JPM) alishauriwa vibaya!

Kauli hiyo ya Ndugai nayo ilipata mashambulizi mengi kwenye majukwaa mbalimbali. Watu walihoji kwa nini kiongozi wa mhimili adhimu wa Bunge alikaa kimya na kuishia kuunga mkono uamuzi wa serikali wa kusitisha ujenzi wa mradi wa bandari ya Bagamoyo? Ni kiongozi huyo huyo alisikika Bungeni wakati wa uongozi wa Magufuli kwamba mradi huo ni wa kitapeli. Iweje leo abadilike na kudai Rais alishauriwa vibaya?

Swali la kujiuliza na ambalo kila mtu amekuwa akijiuliza ni kwa nini viongozi walikaa kimya JPM alipokuwa hai kama si unafiki, undumilakuwili, ukinyonga na roho ya usaliti hiyo?

Ni kwa msingi huu, nasema viongozi wa aina hii ni hatari sana kwa mustakabali wa taifa letu kwa sababu kipindi cha uongozi wa JPM walikuwa (kwa nafasi walizokuwa nazo) na fursa tosha ya kumshauri kiongozi mwenzao.

Ni Kigwangala huyu huyu aliyekuwa akishindana na aliyekuwa Mkurugenzi wa mawasiliano ya Rais Ikulu, Gerson Msigwa na aliyekuwa Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk. Hassan Abbas, kutetea kila tamko la JPM mitandaoni. Pia ni Ndugai huyu huyu aliyesahau kabisa uhuru wa Bunge na kutamka hadharani kuwa JPM akikataa kuongezewa muda "tutamlazimisha!"

Ninavyokumbuka serikali haikufurahishwa na masharti ya China Merchants kuanzia mwaka 2014 na kuvutana nao hadi kipindi cha JPM ambaye hakutaka kupoteza muda zaidi. Akawaambia China Merchants Mwaka 2018 "STOP" kutokana na masharti magumu yaliyoelekea kuiweka nchi rehani kiuchumi na kisiasa.

Wachina ambao Ndugai anawaita ndugu zetu walitaka waendeshe bandari hiyo baada ya ujenzi bila kuingiliwa; jukumu la kuweka tozo liwe mikononi mwao; ukanda mzima wa pwani (toka Tanga hadi Mtwara) usifanyiwe ujenzi wa bandari mpya wala uboreshaji wa bandari zilizopo ili kulinda uwekezaji wa Wachina Bagamoyo; Wachina wapewe umiliki wa miaka 99 wa eneo lote la ujenzi wa viwanda na mji wa kisasa wa Bagamoyo; na -mradi huo ukileta hasara, basi serikali iwe tayari kufidia hasara hiyo!

Hivi kweli, Ndugai hatambui madhara ya masharti haya kwa usalama na ustawi wa nchi? Hivi Ndugai anadhani kuondoka kwa JPM ni fursa ya kurejesha yote ambayo JPM aliyakataa katika kutetea maslahi ya nchi?

## DARASA LA NDOA

# Mambo ya kuzingatia wakati wa uchumba - 3



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Mtu anayeoa au kuolewa kwa kuzingatia kigezo kimoja tu cha mwonekano (physical appearance) anajiweka katika hatari kubwa kimaisha. Mwonekano wa mtu ni jambo la msimu au wakati tu kwani mwanadamu si kiumbe mgando,**

UCHUMBA huanza na urafiki. Mtu anaweza kuwa na marafiki wengi, lakini mchumba huwa ni mmoja tu, ambaye hutokana na marafiki mtu alio nao.

Uamuzi wa kuoa au kuolewa ni muhimu zaidi na mzito kuliko uamuzi wa kununua hivyo nyumba au gari. Ni uamuzi muhimu sana ambao mtu anafanya kuhusu maisha yake, hivyo utulivu, umakini na uongozi wa Mungu vinahitajika ili kumwezesha mtu kufanya uamuzi makini.

Katika sehemu ya kwanza na ya pili ya makala hii, tuliangalia masuala mbalimbali ambayo mtu anapaswa kuyazingatia wakati wa uchumba kabla ya kuingia kwenye maisha ya ndoa.

Sehemu hii ya tatu na ya mwisho ya makala hii, pamoja na mambo mengine, inajaribu kuelezea sababu batili za kutaka kuona au kuolewa. Migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi kwa sehemu fulani vimechangiwa na sababu potofu au batili zilizowafanya watu waingie katika ndoa. Baadhi ya sababu hizo ni:

Tendo la uasi

Baadhi ya vijana wamepishana misimamo na wazazi wao kuhusu watu wa kuwaoa au kuolewa nao. Maoni na ushauri wa wazazi vimepuuzwa. Kwa hiyo, kijana analazimisha na kufunga ndoa na mtu aliyekataliwa na wazazi wake. Ndoa za namna hii huwa hazidumu kwa sababu ya kukosa baraka za wazazi.

**MVUTO WA NJE**

Mtu anayeoa au kuolewa kwa kuzingatia kigezo kimoja tu cha mwonekano (physical appearance) anajiweka katika hatari kubwa kimaisha. Mwonekano wa mtu ni jambo la msimu au wakati tu kwani mwanadamu si kiumbe mgando, hubadilika kutokana na sababu mbalimbali za kibaiolojia, maumbile na mazingira.

**LENGO LA KUREKEBISHWA**

Kuna vijana wameoa au kuolewa na watu ambao wakati wa uchumba walishindwana katika mambo fulani. Kwa sababu ya kulewa mapenzi, wakaoana vivyo hivyo kwa matazamio kuwa mtu atabadilika akiishaingia kwenye ndoa. Mara nyingi mambo yamekuwa kinyume na matazamio. Ndoa za namna hii hudumu kwa muda mfupi sana.

**TAMAA YA FEDHA**

Fedha si jawabu la matatizo yote ya binadamu. Fedha inapokuwa kipaumbele na kigezo pekee cha mtu kuoa au kuolewa, ndoa ya namna hii iko katika hatari ya kufa muda wowote, hasa pale fedha zitakapokosekana au zitakapopungua. Uhusiano unaojengwa katika msingi wa fedha huwa haudumu.

**UNAFUU WA MAISHA**

Wako vijana wametamani kuingia katika ndoa ili kuepukana na hali ngumu ya maisha ya nyumbani kwao. Hoja ya msingi hapa ni kutoka. Ndoa inachukuliwa kuwa suluhu ya matatizo.

Ni hatari kuingia katika ndoa kwa mtazamo huu, kwa sababu vijana wengi wamejikuta katika matatizo makubwa zaidi baada ya kuoa au kuolewa, kiasi cha kukumbuka nyumbani walikotoka. Walidhani wameyakimbia matatizo, kumbe wameyatafuta.

**TIBA YA MAJERAHA**

Uhusiano wa awali unapovunjika, watu wengi wamejikuta wakianzisha uhusiano mpya wangali na machungu au maumivu nafsini, kiasi cha kuharakisha kuingia katika ndoa. Machungu/maumivu yameleta msukumo ndani ya mtu wa kutaka kuoa/ kuolewa.

Msukumo wa namna hii huondoa umakini wa mtu. Kwa hiyo, watu wengi wamejikuta katika maumivu zaidi na kukosa walichotamani kukipata. Uhusiano wa namna hii huwa haudumu kwa muda mrefu. Ni muhimu uhusiano mpya uanze ukiwa umepona majeraha ya uhusiano uliopita.

Ingawa ndoa zilizoanza kwa sababu batili zinaweza kuwa na uhusiano wenye furaha, ni muhimu kuzingatia kuwa, uhusiano usiojengwa katika msingi wa upendo, uko katika hatari kubwa ya kuvunjika.

**HITIMISHO**

Mafanikio katika maisha ni matokeo ya maamuzi mtu anayofanya na jinsi anavyoutumia muda wake. Maisha yanahitaji utaratibu, uvumilivu, subira, utulivu na nidhamu katika kile kinachotafutwa. Marafiki na mchumba huchaguliwa. Uamuzi wa kuoa au kuolewa ni muhimu na mzito. Ni uamuzi unaohitaji utulivu na umakini mkubwa, kwani ni uamuzi unaohusu maisha mazima ya mtu.

Ndoa si taasisi ya kuivamia, bali maandalizi yanahitajika. Bahati mbaya sana, watu wengi huelekeza nguvu kubwa katika kuandaa sherehe kubwa za harusi, badala ya kujiandaa kuwa mume au mke bora. Kwa hiyo, ni muhimu wanandoa watarajiwa wafahamu mahitaji na madai ya taasisi ya ndoa kabla ya kufanya uamuzi wa kuingia katika ndoa.

**Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255 744000066.**

# MAISHA

APRILI 18, 2021
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 10


## Hana adabu, mzazi unahusika



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Tambua haya unapofunga kamba za nguo nyumbani



## HARUSI

Ukurasa 12



# Raha ya ukwaju katika urembo

Ukurasa 14

# Hana adabu, mzazi unahusika

Na Moses Ismail



NDIPO tulipofikia sasa malezi ya kisasa yanatugharimu, yanasababisha vijana wenye adabu kuwa kama ‘bidhaa’ adimu!

Hayo ni maneno ambayo ninayawaza nikiwa ndani ya mwendo kasi baada ya kijana mmoja kuinuliwa na sauti zenye kufoka kutoka kwa baadhi ya abiria waliokuwa karibu naye.

Abiri hao walilazimika kumfokea kijana huyo baadaya kung’ang’ania kukaa kwenye kiti ambacho siyo kwa ajili yake.

Kwa kawaida ndani ya mabasi hayo ya mwendo kasi kuna viti kadhaa vikiwamo vilivyotengwa maalum kwa ajili ya wazee wajawazito, walemavu au wagonjwa.

Kijana huyu mwenye mwonekano wenye afya nzuri baada ya kupanda kwenye basi lile na kubaini viti vyote vya kawaida vimejaa akaamua kukaa kwenye viti hivyo maalum.

Lakini baada ya kukaa tu, akapanda baba mmoja mzee akiwa amechoka, kijana akajikausha pale, tena akatoa simu yake na kuanza kubofya bofya wenyewe wanaita kuperuzi!

Kitendo hicho baadhi ya abiria walikiona wakajaribu kumwambia kwa ustaarabu ili apishe lakini akajifanya asikii kang’ag’ana na kuperuzi, jambo ambao lilisababisha watu hao kupandwa na hasira na kuanza kumshambulia kwa maneno makali.

Kijana alikuwa mwenye kiburi haswa kwani hadi dereva wa lile basi alilazimika kumfuata na kumwamuru asimpishe yule mzee ndipo akasimama, akiwa amefura kwa hasira.

Ndipo aliponifanya nijikute nikizungumza na nafsi yangu kwamba nipo tulipofika, mmomonyoko wa maadili hadi tabia njema imekuwa ni shida.

Hii siyo mara kwanza kuona jambo hili mara kadhaa nimejionea hivyo, wakati mwingine kile kiti kinajaa wenye uhitaji unakuta bado kuna wengine wamesimama lakini vijana wamekaa kwenye viti bila shaka.

Nimewahi kulazimika kusimama mimi kupisha mlemavu kukaa wakati kulikuwa na abiria wenye umri mdogo wana afya nzuri lakini hawapo tayari kupisha.

Mambo kama haya yanatakiwa kudhibitiwa, kijana siku zote anapaswa kuwa shupavu na siyo legelege kiasi cha kuona shida kusimama kupisha mlemavu, mjamzito au mlemavu kukaa kwenye siti.

Mafunzo yanatolewa kuanzia kwenye ngazi ya familia, shuleni, kwenye nyumba za ibada jinsi gani kijana anapaswa kuwa mfano bora kwa jamii ikiwamo kuwahurumia watu wenye uhitaji.

Ingawa kuna uwezekano mkubwa kuwa msingi wa malezi unaanzia nyumbani na baadhi ya wazazi wamekuwa wakichangia kuwalea vibaya watoto, ikiwamo kushindwa kuwafundisha muhimu wa kuwa na huruma kwa wenye uhitaji.

Kukosa huruma kwa watu wa namna hiyo ni ukatili kwa kuwa tu mwenye afya njema anapaswa kusaida wenye uhitaji kwa hali na mali, kama haiwezekani kuwajali kwa hali zao ni wazi hawawezi kuwasaidia kwa kuwapa (sadaka) mahitaji yao muhimu pale inapobidi.

Nimeshuhudia hata baadhi ya wanafunzi hukimbilia kukaa kwenye viti na kufunika nyuzo zao wakiigiza kulala, hawapishi watu wazima kuwa kwenye viti hivyo, ni vyema wakatafakari kama wao wanachoka kwa kukaa darasani na kufundishwa vipi huyo mtu mzima, ambaye anakabiliwa na majukumu mengi kuliko.

Kukaa kwenye viti ni haki ya kila abiria lakini kwa hali ilivyo kwenye magari hayo wapo wanaopaswa kusimama, lakini pia hata kwenye daladala, vijana wanapaswa kuonyesha ushupavu wao badala ya kuwa legelege huku wengine wakiwa hawana hata muda wa kufanya mazoezi.

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

Weka maneno yafuatayo katika mtitiriko utakaoyafanya yalete maana kamili.
Mfano: **marguerite/est/La/fleur/une**
-La marguerite estune fleur.

oiseau/Le/un/est/perroquet
………………………………………………….

plantesfragiles/Les/rosiers/des/sont
………………………………………………….

un/saumon/poisson//est/Le
………………………………………………….

est/erable/arbre/un/L’
………………………………………………….

citron/est/Le/fruit/un
………………………………………………….

poireau/un/est/Le/legume
………………………………………………….

des/Le chien et le chat/animaux-domestiques/sont
………………………………………………….

bambou/une/Le/est/herbe
………………………………………………….

qui/méne au success/est/Le/un/pont/fragile
………………………………………………….

c’est/l’histoire/qui commence/Entre/au depart/nous
………………………………………………….

d’avoir/Sois/raison/et puis/sûr/vas-y
………………………………………………….

la durée/le soleil/de la nuit/apparaîtra/Quelquesoit
………………………………………………….

Jibu kama kwenye huo mfano hapo chini.
Mfano: **Tu as une valise?** – Oui, j’aiune valise de mon frère.

Vousavez des chaussures de marche? – Oui, j’ai…….chaussures de monpère.

Tu as un appareil photo? – Oui, j’ai……….appareil photo de moncopain.

Vousavezunetente de camping? – Oui, j’ai………….tente de mon cousin.

Tu as unevoiture? Oui, j’ai……..voiture de mes parents.

Tu as des skis? – Oui, j’ai…….skis de ma sœur.

Vousavezun sac à dos? Oui, j’ai……..sac à dos de ma tante.


Tu as unstylo? Oui, j’ai……..stylo de monvoisin.

Vousavezuneboisson à consommer? Oui, j’ai…….boisson de ma petite amie.

Tu as des lunettes? Oui, j’ai……..lunettes de monami.

## WATOTO

## PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

JAMAA mmoja alianguka kutoka kwenye gorofa ya pili hadi chini. Haraka watu walikusanyika na kutaka kumsaidia.

Mmoja alimuuliza vipi imekuaje hadi unaanguka?

Yule jamaa huku akiugulia, alimjibu hata mimi sijui ndo kwanza nafika sasa hivi,”

Watu “Haaa jamaa sio mzima huyu.”

**SWALI**
Heka moja ina wastani wa mita ngapi?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Vijue vita anavyopaswa kupigana mwanadamu katika maisha yake

KARIBU tena msomaji wangu katika safu yetu ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Tayari tumeona mfano wa mtu ambaye hatua zake za mafanikio zimefungwa. Kila anapojaribu kusonga mbele hawezi. Nikasema pia kwamba mwenye nguvu atamshinda aliye dhaifu.

Hivyo vyote ni vita ambavyo inahitajika mbinu thabiti ili uweze kuwa mshindi. Ni ukweli usiopingika kwamba ushindi mkubwa wa vita yoyote kwenye maisha ya mwanadamu hupatikana kwa maombi mazito ya upenyo.

Hata maandiko ya Mungu yanaonyesha wazi kuwa vita ilikuwepo tangu siku ile mwanadamu alipomuasi katika bustani ya Edeni. Kuna mambo kwenye maisha huwezi kuyapata kama hujapigana vita vya kiroho.

Msomaji wangu, kwenye maisha kuna vita mbalimbali vya kupigana ili kuona upenyo. Na kama hutavishinda, unaweza kushangaa maisha yako yakiharibika na kushindwa kutimiza ndoto zako. Baadhi ya vita hivi ni vifuatavyo;-

Kwanza, viko vita vya kufika kwenye hatima yako iliyotukuka. Kila mtu anayekuja duniani anakuwa na kusudi maalum la kutimiza. Hakuna mtu ambaye Mungu amemleta duniani bila kusudi. Lakini ili uweze kulitimiza lazima upigane vita.

Ili kutimiza ndoto zako kwa kufikia viwango vya juu vya taaluma au utumishi wako ni lazima upigane vita. Ukiona ndoto zako hazijatimia na umri unakwenda, usiishie tu kulalamika, fanya kitu, chukua hatua.

Ukiona umetumia akili na nguvu zako zote bila mafanikio, usikae tu na kuanza kulaumu watu wengine. Pigana vita vya kiroho. Huenda chanzo chako kutofanikiwa kikawa kiroho zaidi.

Pia kuna vita vya kuwa na familia yenye ushindi. Hapa ni lazima upigane. Huwezi kuwa na familia yenye ushindi kama hujui siri ya kupigana vita vya kiroho.

Kwenye ulimwengu huu ulitawaliwa na kila aina ya nguvu za giza, mapepo, majini ni lazima ufahamu siri hii ya kupigana vita vya kiroho. Kwa mfano kabla hujaoa au kuolewa ni lazima upigane vita vya kiroho ili upate mke au mume wa hatma yako.

Watu wengi leo walioko kwenye ndoa wanalia sana na wengine wanajuta kwa maamuzi waliyoyafanya wakati wa kuoa au kuolewa. Wengine hawakuwa na muda mrefu wa kumuomba Mungu kwa habari ya wenzi wao (partner).

Wengi walikurupuka tu. Wengine waliruhusu hisia zao kwa wakati ule ziwachagulie wenza. Wengine walivutiwa na muonekano wa nje bila kusikiliza mapenzi ya Mungu kuhusu mahusiano yao. Wengine walijikuta wakioa au kuolewa kwa sababu ya vitu, mali na sasa wanajuta.

Zamani katika Israel, kabla binti hajaolewa. ilikuwa lazima aende milimani kwa miezi miwili kumlilia Mungu kwa habari ya ndoa yake. Na kabla hujapata watoto ni lazima upigane vita ili uwe na watoto wenye sifa njema.

Leo vilio vingi kwenye familia ni kwa sababu wazazi walishindwa kupigana vita magotini, walishindwa kufanya vita dhidi ya misingi mibaya iliyoharibu watoto. Walishindwa kupigana dhidi ya mapepo yanayosababisha utasa, dhidi ya roho zinazoharibu watoto.

Mtoto ana haki ya kujengewa misingi bora ya malezi. Mzazi asipotimiza hilo, mtoto akaharibika atamlaumu nani?

Mpenzi msomaji, ni muhimu usimame na uipiganie familia yako. Ni kweli unaweza usiwe na nguvu za kimwili za kupigana, lakini una nguvu za kiroho na ukipigana kwa bidii na kwa imani utashangaa ukiona Mungu atakavyokushindia.

Pia iko vita ya kuwa na uchumi mzuri. Unaweza kuwa na akili nzuri, kiwapa kikubwa, karama kubwa, uwezo mkubwa wa kufanya kazi, taaluma nzuri lakini ukashangaa kuwa na uchumi mbaya. Hivi hujawahi kuona wataaamu kwenye masuala ya uchumi wakipambana kuwa na uchumi mzuri?

Ili uwe na uchumi mzuri hupaswi kuwa na elimu tu , au karama, bali unahitaji kuwa na nguvu ya kumiliki. Na nguvu hii inaanzia kwenye ulimwengu wa roho. Unapochukua uamuzi wa kuitafuta nguvu hii kwa imani na kwa bidii kupitia maombi, utashangaa kuona ikifanya kazi juu yako na kukuletea faida ya ajabu.

Vile vile vipo vita vya kuwa na afya nzuri. Upo wakati utapata mtikisiko wa kiafya au miongoni mwa wanafamilia, mshirikishe Mungu. Vita nyingine ni ushawishi. Dunia imejaa vishawishi, lazima uvishinde. Pia ipo vita ndani ya mtu kama vile hasira ya ghafla, huzuni, chuki, upweke, kujikataa na kadhalika.

***Msomaji wangu, niishie hapa tukutane wiki ijayo kwa neema ya Mungu. Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Tumuunge mkono Rais Samia nchi ni yetu sote

NI mara ya kwanza kwa Tanzania kupata msiba wa Rais aliyeko madarakani. Jambo hili limekuja kwa mshtuko mkubwa na hofu kwamba hali itakuwaje na kama tutavuka salama.

Hata hivyo, tumefanikiwa kuvuka salama kihunzi cha kutimiza matakwa ya kikatiba kwa amani kabisa. Sasa Rais Samia Suluhu Hassan anaunda serikali yake kwa kupanga safu ya uongozi kwa mujibu wa katiba na tayari ameshafanya uteuzi na mabadiliko mbalimbali.

Rais Samia katika hotuba zake, ameonyesha dira ya serikali yake kuwa ni umoja na kuondoa uonevu wa aina yoyote ndiyo maana bila hofu alieleza kuwa hatataka kodi ya dhuluma huku akiitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuacha ubabe ambao unaua biashara.

Alikwenda mbali zaidi na kuruhusu uhuru wa vyombo vya habari huku akitaka vilivyofungiwa kufunguliwa ili vifanye kazi, jambo ambalo limepokewa kwa furaha kubwa na waandishi wa habari ambao wengi hawana kazi kutokana na vyombo kufungwa au kushindwa kujiendesha.

Katika hotuba yake ya kwanza, alihuburi mshikamano, upendo na umoja wa kitaifa. Kama haitoshi, alitaka uwazi hasa kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), hasa kwenye mashirika ya umma.

Tayari Ripoti ya CAG imewasilishwa bungeni kwa mujibu wa sheria lakini kinachoonekana bungeni ni wabunge wa chama kimoja kusigana, kurushiana maneno, kuzodoana na kuumizana kwa maneno hadharani.

Nikiwa mtazamaji na mfuatiliaji wa bunge, naliona kundi la wabunge wanaotaka yaliyoanzishwa na Hayati Rais John Magufuli yaendelezwe na yatajwe mara kwa mara kama rejea ya mambo anayofanya Rais Samia.

Wako wengine wanaosema kila kitabu na zama zake na siku zote alama ya kiongozi inajitetea na si lazima wawape wa kuitetea, huku wakitaka wanaoteta wasione shida kuambiwa kuna eneo haikuwa imekaa sawa na wale wanaoona kila kitu kiko sawa wakifurahia wasichukiwe.

Wananchi wanachotarajia kusikia ni kubishana kwa hoja na si kurushiana maneno makali. Kinachoonekana kwa sasa ni mgawanyiko kwamba nani kasema nini na ajibiweje na si nani kasema nini chenye maana ili ajibiwe kwa misingi ya alichokisema pasipo kumuumiza.

Ni muhimu sana Rais Samia akaachwa atekeleze wajibu wake kwa mujibu wa katiba pasipo shinikizo lolote huku tukijua kuwa amekalia kiti hicho kwa mujibu wa katiba na ana mamlaka kamili.

Haipendezi kuona anapangiwa au kushinikizwa kuenenda kwa kadri ya matakwa ya watu wa kundi fulani ambao wanasahau kuwa Tanzania ni mali ya wenye vyama na wasio na vyama.

Kwenye uchaguzi mkuu, wako waliopiga kura, ambao hawakupiga, wenye vyama na wasio na vyama na kwa mujibu wa katiba yetu, wote wanaongozwa na Rais aliyechaguliwa na hao waliopiga kura.

Ninatarajia Rais Samia atapata ushirikiano mkubwa ndani ya chama chake na kisione shida pale atakapofanya marekebisho ya mambo yaliyofanywa na mtangulizi wake kwa kuwa si wa kwanza kufanya hivyo. Hakuna kiongozi aliyetoka madarakani alifanya mabadiliko na likaibuka kundi kumlazimisha aendeleze ya mtangulizi.

Kwa sasa wabunge wa CCM ndio wanabishana na kurushiana maneno ambayo wakati mwingine yanatuma salamu mbaya kwa umma. Hii haifai bali wamuunge mkono Rais na si kunyooshena vidole na kuonenana wako wasaliti na wafia nchi.


Ubaguzi huo hautaishia bungeni bali utakwenda hadi kwa jamii ambayo sasa itabaguana kwa vyama, kundi la Rais JPM na la Rais Samia na mwisho hatutakuwa na nchi bali vipande vipande. Ni muhimu sana wanasiasa wachunge ndimi zao wasije wakaliangamiza taifa.


Ni wakati wa kumwombea Rais Samia ili aliunganishe taifa na kusimamia vizuri maendeleo ya nchi ambayo yatatunufaisha sote na kusiwe na namna yoyote ya kumjaribu.


Ndiyo maana Ramia alisema ni muhimu sana ikatambulika kuwa yeye ndiye Rais wa Tanzania, Rais mwenye maumbile ya mwanamke. Hata siku moja maumbile yasionekane ni sababu ya kumjaribu aliyepewa mamlaka kwa mujibu wa katiba.

# HARUSI













**ILIKUWA** ni siku ya furaha kwa ndugu na jamaa wa Ibrahim Moshi baada ya kufunga ndoa na Fatma Hussein Aprili 9, mwaka huu, eneo la Kipawa ikifuatiwa na sherehe ya kuwapongeza katika Ukumbi wa Tazara jijini Dar es Salam. (Kwa watakaopenda picha zao za harusi zitoke kwenye ukurasa huu wawasiliane kwa namba: 0717336368 au barua pepe: Moshilusonzo@Gmail.com)

MITINDO

# Mwendo wa kanga, Maclenzie

WIKI iliyopita tulikuwa na uwanja mpana wa kuelezea namna unaweza kutoka vizuri ukiwa na mavazi ya Kiafrika zaidi.

Tulieleza namna nguo aina ya Kitenge na Bazee zinazoweza kumnogesha mtu pale anapotaka kwenda sehemu yoyote ile.

Leo tunaendelea na uelimishaji kuhusu umuhimu wa kuvaa mavazi ya kiafrika kama njia ya kujitukuza na kujitofautisha na wengine.

**MACKENZIE**

Nguo za Mackenzie zinafahamika kiasi kidogo hasa kwa kizazi cha sasa, lakini ni moja ya vazi linalopendeza na kumfanya mtu kutoka kiafrika zaidi.

Vazi hili limepata umaarufu miaka ya nyuma, lakini linaendelea kupendwa na baadhi ya watu baada ya wabunifu kulitumia mara nyingi katika maonyesho ya mitindo ya nguo.

Kwa kawaida Mackenzie ina mchanganyiko wa rangi nyingi na maua yanayopendeza kuangalia. Unapochanganya na vitambaa vingine ndivyo ladha yake huongezeka zaidi.

**KHANGA**

Vazi hili limepata umaarufu katika ukanda wa pwani, mara nyingi watu huita kama fahari ya maneno na vichambo.

Hii ni kutokana na aina ya upambaji wake unavyokuwa ,maua yenye rangi tofauti, ukubwa unaojitosheleza na ujumbe wa maneno chini ya khanga.

Khanga ina matumizi ya aina nyingi, dadi kubwa ya maisha ya wanawake nchini hutumia vazi la khanga kama kujifunga,kubebea watoto, kushona gauni au aina nyingine ya vazi.

Kwa wanaume vazi hili linapata nafasi ya kutumika pale anapotaka kujifunga wakati anakwenda kuoga ,kushona mashati, kaptula na suruali.












UREMBO



# Raha ya ukwaju katika urembo

TUNDA la ukwaju linafahamika na watu wengi kutokana na kupatikana sehemu nyingi.

Licha ya kupatikana kwa urahisi, idadi kubwa ya watu hawapendi kula pengine kutokana na ladha yake ya uchachu pamoja na usumbufu wa kuchubua ulimi pale unapokula kwa wingi.

Hata hivyo, tunda hili lina faida kubwa kwa wanawake wanaopenda urembo, kwani husaidia kuufanya mwili kuwa imara kwa kupunguza uzito, kuboresha afya ya nywele pamoja na ngozi.

Pia ukwaju huondoa weusi kwenye shingo, kutibu chunusi na kutibu ngozi ya kichwa yenye mafuta.

Jinsi ya kutumia ukwaju kwa ajili ya ngozi

**KUNG'ARISHA NGOZI**

Unatakiwa kuchukua matunda ya ukwaju gramu 30, maji ya moto nusu lita na manjano nusu kijiko cha chai.

Unatakiwa kuloweka tunda za ukwaju katika maji ya moto kwa dakika kumi, halafu toa mbegu ili kubaki juisi kabla ya kuchanganya na manjano.

Paka mchanganyiko wako katika uso wako na uache kwa dakika 15, kisha osha kwa maji ya vuguvugu. Unapotaka kuondoa weusi kwenye shingo, unatakiwa kuongeza juisi yako ya ukwaju na kijiko kimoja cha asali na kijiko kimoja cha maji waridi 'rose water'.

Changanya vizuri paka shingoni na uache kwa dakika 20, kabla ya kuosha kwa maji ya uvuguvugu.

Katika kutibu chunusi usoni, changanya juisi ya ukwaju na kijiko kimoja cha mtindi na manjano kijiko kimoja. Mchanganyiko huu unatakiwa kupaka usoni na unalazimika kukaa mpaka ukauke vizuri.

Ukiona umekauka osha uso kwa maji ya vuguvugu na paka mafuta kwa ajili ya kulainisha ngozi

Fanya hivi mara mbili kwa wiki tu ili kukupa ngozi laini na yenye afya.









MAPISHI

Na Mary Geofrey



# Uji wa tangawizi mbichi

TUKIWA ndio kwanza tupo katika msimu wa mfungo wa ramadhan, katika futari, uji ndio chakula pekee kinachoongeza hamu wakati wa kufuturu.

Kutokana na umuhimu wake, leo tutajifunza namna ya kupika uji wa tangawizi mbichi.

**MAHITAJI**

Unga wa ulezi wa mchanganyiko mbalimbali, dona au unga wowote uupendao kwa uji.

Maziwa nusu lita, sukari au asali na tangawizi mbichi iliyosagwa kijiko kimoja cha chakula.

Maji lita moja na nusu, siagi kijiko kimoja cha chakula au mafuta ya kupikia.







**NAMNA YA KUPIKA**

Weka maji katika sufuria yako, weka tangawizi iliyosagwa kwenye maji, unaweza ukachuja tangawizi ili kuondoa makapi kama hupendi kuyasikia wakati unakunywa uji.

Weka unga vijiko saba vya chakula kabla maji hayapata moto ili kuepuka mabuja katika uji wako huku ukiendelea kukoroga.

Ongeza maziwa yaliyochemshwa kwenye uji wako kama uji ni wa ulezi hakikisha umeiva ndipo uongeze maziwa na sukari uipendayo au sali kwenye uji wako.

Endelea kukoroga na uache jikoni kwa dakika 15 na utakuwa tayari umeiva, uepue na tenga mezani kwa ajili ya wanywaji.

Uji huu unatumiwa na watu wazima na watoto kama wanatumia tangawizi.

## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# Tambua haya unapofunga kamba za nguo nyumbani



UTUNZAJI wa mazingira ya nyumba ni uwanja mpana ambao unabeba mambo mengi yanayohusisha moja kwa moja ustawi wa nyumba au nyumbani.

Miongoni mwa mambo yanayohusisha nyumba ni pamoja na utunzaji wa mazingira ikiwamo kila kitu kilichomo katika nyumba hiyo ndani na nje kwa kuhakikisha kinawekwa katika mpangilio mzuri ambao unaleta mvuto.

Nje ya nyumba, yako mambo mengi yanapaswa kuzingatiwa, iwe ni kwa ajili ya mapambo au kwa ajili ya matumizi ya watu wanaoishi katika nyumba.

Yote kwa ujumla wake yanatakiwa yawekwe katika mpangilio sahihi ambao hauharibu mwonekano au mvuto wa nyumba.

Pamoja na hayo, leo napenda nizungumzie namna ya kutengeneza kamba ndani ya ua wa nyumba kwa ajili ya kuanika nguo bila ya kuharibu mvuto au mwonekano wa nyumba.

Kamba ni miongoni mwa mahitaji muhimu kwa matumizi ya watu wanaoishi ndani ya nyumba kwa sababu suala la kufua nguo halikwepeki.

Suala hili tunaweza kuliona la kawaida lakini kutokana na tathmini yangu ndogo katika baadhi ya nyumba, nimejifunza kwamba wengine tunashindwa kulizingatia hususani kwa kupenda kutengeneza sehemu ya kuanikia nguo inayoharibu mwonekano wa nyumba kabisa.

Mtu anaweza kuwa na nyumba nzuri lakini akashindwa kutafuta sehemu nzuri ya kuweka kamba ya kuanikia nguo. Badala yake anaweka hata katika sehemu ya lango kuu la kuingilia, hivyo hata wageni wanapoingia wakati mwingine nguo zinapeperushwa na upepo na kuwaangukia kwa bahati mbaya au kuzagaa ovyo.

Pia ni muhimu tuwe na kamba bora za kuanikia nguo kwa ajili ya kulinda mvuto wa nyumba badala ya kuokoteza ilimradi tu nguo zianikwe na zikauke na kuanuliwa.

Unapofunga kamba katika eneo sahihi lisiloharibu muonekano wa nyumba na zikawa ni nzuri, nazo zinachangia kwa kiasi fulani kupendezesha mazingira ya nyumba husika.

Baadhi ya kamba kutokana na ubaya au kwa sababu zinaachwa na kuchakaa na kutokuwekwa katika eneo sahihi. Pia zinapokuwa hazijaanikiwa nguo, huharibu mwonekano na kuonekana kama uchafu katika nyumba.

Baadhi yetu tunaungaunga kamba za rangi za ajabu tena wengine ni za vipisi vya nguo au vitambaa, hivyo kuleta picha mbaya au kuonekana kama uchafu kwenye nyumba.



## Dondoo ya kuhakikisha unachagua vioo sahihi kwa madirisha ya nyumba yako

**1:** Chagua aina ya vioo ambavyo vina unene mkubwa ambao unazuia kuvunjika haraka endapo itatokea mitikisiko au kupigwa na vitu kwa bahati mbaya.


**2:** Kwa wanaoishi sehemu za baridi wantakiwa kuchagua kioo ambacho hakiingizi hali ya hewa ya baridi ndani. Pia kama hutaki mwanga, chagua vioo vyenye giza.

**3:** Hakikisha Flemu zinazoshikilia vyoo ni imara, epuka kununua vyuma feki ili kutokupatia gharama ya ukarabati kila mara.

**4:** Kitu cha muhimu chunguza kioo kama kimetengenezwa na kampuni inayotambulika, kwani kuna aina nyingi za vioo ambavyo si imara.



# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO...

...MWENYE NYUMBA HADAIWI KODI

# Marekani, Urusi zatunishiana misuli

**Moscow,** Urusi

NCHI za Urusi na Marekani zimeingia katika mvutano mwingine wa kidiplomasia, baada ya kila upande kuwatimua maofisa wa balozi.

Jana Urusi ilitangaza kuwafukuza wanadiplomasia 10 wa Marekani na kuwataka kuondoka nchini humo kama hatua ya kulipiza kisasi baada ya Marekani kuwafukuza wafanyakazi 10 wa Urusi kwa madai ya udukuzi na kuingilia uchaguzi wa Marekani.

Wizara ya mambo ya nje ya Urusi ilisema John Sullivan, ambaye ni balozi wa Marekani nchini Urusi, anatakiwa kuondoka nyumbani katika kile walichosema ni kwa mashauriano zaidi.

Kupitia taarifa, wizara ya mambo ya nje ya Urusi ilisema huu ni wakati wa Marekani kuonyesha ukomavu wa kiakili na kugeuza mkondo wao wa kugombana. Taarifa hiyo iliongeza kuwa ina uwezo wa kuiumiza zaidi Marekani kuichumi na kupunguza idadi ya wanadiplomasia wa Marekani nchini humo humo hadi 300, japo kwa sasa haitachukua hatua hiyo.

Uamuzi huo ni sehemu ya mpango mpana wa kulipiza kisasi, uliidhinishwa na Rais Vladimir Putin kama jibu kwa Marekani baada ya serikali ya Joe Biden kuiwekea vikwazo Urusi.

Hata hivyo, nchi hiyo ilijibu haraka na kuweka hatua ambazo zinanuia kupunguza ushawishi wa Marekani nchini humo, Urusi imeacha mwanya wa mazungumzo uliopendekezwa na Rais Joe Biden aliyetaka kufanyika mkutano kati yake na Putin ili kujadili masuala kadhaa.

Marekani imeituhumu Urusi kwa udukuzi na kuingilia uchaguzi wake

Hata hivyo, ilisema vikwazo ilivyoiwekea Urusi ni jibu lake kwa Urusi baada kuingilia uchaguzi wa mwaka jana wa Marekani, kufanya udukuzi, na kuitishia Ukraine pamoja na vitendo vyengine.

Madai hayo yamekanushwa na Urusi imekanusha madai yote dhidi yake.

Vile vile, ofisi ya Rais Putin bado haijaamua iwapo atashiriki katika mkutano wa kujadili athari za mabadiliko ya tabia nchi unaoongozwa na Marekani wiki ijayo.

Ikulu ya Kremlin imeongeza kusema, itakuwa vigumu kuandaa kwa haraka mkutano wa kilele baina ya Putin na Biden.

Msemaji wa Ikulu Dmitry Peskov, alisema juzi kuwa Putin kwa muda mrefu amezungumzia juu ya umuhimu wa kurejesha uhusiano wa kawaida na Marekani.

Peskov alisema "Ni vizuri kuwa viongozi hao wawili wamekubaliana juu ya hili." Hata hivyo, msemaji huyo alishtumu vikwazo vipya vilivyowekwa na Marekani.

Uhusiano kati ya Urusi na Marekani umetetereka katika siku za hivi karibuni baada ya Rais Biden kusema kuwa anadhani Putin ni muuaji.

**DW**



Kikosi cha askari kikiwa ndani ya mlango mkuu wa Kasri la Windsor,wakijiandaa na gwaride la mazishi ya mume wa Malikia Elizabeth wa Uingereza, Prince Philip, jana.

# Eritrea yakiri vikosi vyake viko Ethiopia

**ASMARA,** Eritrea

ERITREA imekiri kwa mara ya kwanza kwamba wanajeshi wake wanashiriki katika vita vya Mkoa wa Kaskazini mwa Ethiopia wa Tigray.

Hata hivyo nchi hiyo imetoa hakikisho la kuwaondoa baada ya kuongezeka kwa shinikizo la kimataifa.

Hatua ya mwanzo ya kukubali kwa uwazi kuwajibika kwa Eritrea katika mapigano hayo, iliwekwa wazi katika barua iliyosambazwa katika mtandao siku ya Ijumaa na waziri wa habari wa nchi hiyo, iliyoandikwa na balozi wake wa Umoja wa Mataifa na kuelekezwa kwa Baraza la Usalama.

Barua hiyo ilieleza wapiganani wa TPLF walizuiwa kwa kiasi kikubwa na serikali za Eritrea na Ethiopia na zimekubaliana kuanza kuondolewa kwa vikosi vya Eritrea.

Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, aliwapeleka wanajeshi katika eneo la machafuko la Tigray mnamo Novemba kwa lengo la kuwapokonya silaha na kuwadhibiti viongozi wa chama cha kisiasa kilichokuwa kikitawala katika mkoa huo, Tigray People's Liberation Front (TPLF).

**DW**

## Wahamiaji 41 wafa maji Tunisia

**TUNIS,** Tunisia

JUMLA ya wahamiaji 41 wamekufa baada ya boti waliyokuwa wakisafirinayo kuzama katika eneo la bahari la Pwani ya Tunisia.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Umoja wa Mataifa, watu watatu pekee, ndio walifanikiwa kuokolewa.

Mashirika ya kusaidia wahamiaji la IOM na UNHCR yalisema tukio la kuzama kwa boti hiyo lilitokea jioni ya Alhamis katika pwani ya mji wa Sfax.

Awali walinzi wa pwani walisema wahamiaji 20 kutoka katika eneo la kusini mwa Jangwa la Sahara walizama majini.

Msemaji wa walinzi katika eneo hilo, Ali al-Ayari, aliliambia shirika la habari la Ujerumani (DPA) kwamba miili ya wanaume 10, wanawake tisa na mtoto mmoja iliopolewa.

**DW**

## Mapigano mapya yazuka Msumbiji

**PALMA,** Msumbiji

MAPIGANO mapya yametokea katika mji wa Palma, katika jimbo la Cabo Delgado, kaskazini mashariki mwa Msumbiji. Mapigano hayo yalitokea baada ya kupita wiki tatu tangu kufanyika kwa shambulio kutoka kwa kundi la wanajihadi ambalo lilisababisha vifo vya watu wengi na maelfu kutoroka makaazi yao.

Rais wa Msumbiji, Filipe Nyusi, wiki iliyopita alisema vikosi vya serikali vimewafukuza wanamgambo hao wa Kiislam katika mji wa Palma na kwamba wengi miongoni mwao waliuawa.

Mji huo na viunga vyake vinaonekana kuwa chini ya vitisho kutoka kwa wanamgambo hao na katika tukio hilo jipya mashambulio yalisikika katika maeneo mawili yenye umbali wa kilomita 200.

Sehemu muhimu katika mkoa huo, Palma iko kilomita chache kutoka eneo kunakoendeshwa mradi mkubwa wa gesi unaosimamiwa na kampuni ya Ufaransa ya TOTAL.

**RFA**

MAKALA

# UMOJA NDANI YA CCM HUJENGWA NA UPINZANI



Na Magabilo Masambu

**CCM miaka yote ambapo wabunge wa vyama vya upinzani wamekuwapo bungeni, walionekana wamoja na imara katika kuchangia na kupitisha hoja.**

ZANZIBARI ikijitenga kutokana na ulevi tu, 'sisi Wazanzibar na wao Watanganyika'. Wakumbuke kwamba Muungano ndio unaowafanya waseme, sisi Wazanzibari, wao Watanganyika. Nje ya Muungano hawawezi kusema hivyo, kuna wao Wapemba na sisi Waunguja. Nataka mjue hivyo, nje ya Muungano hakuna 'sisi Wazanzibar' wao Watanganyika. Hakuna, kinachowafanya wajiite 'sisi' ni ubaguzi wa kuwabagua Watanganyika, wakiisha wabagua Watanganyika ile dhambi ya ubaguzi haifi inaendelea.

"Dhambi ya ubaguzi ukisha kuitenda inaendelea ni kama ukila nyama ya mtu utaendelea kuila tu. Ninachosema kwa Wazanzibar nakisema pia kwa Watanganyika. Hamuwezi mkakaa salama baada ya kutenda dhambi ya kuwabagua watu wa nchi yenu ileile. Moja, mkawaita wale na ninyi sisi, dhambi ile haiishii hapo. Ndivyo historia ilivyo ni sheria ya historia si historia ya Mwalimu Nyerere. Huwezi kufanya ubaguzi namna hiyo, halafu dhambi ile ikuache hapo hapo. Hapana itakuandama."

Maneno haya Mwalimu Julius Nyerere aliyazungumza katika hotuba yake, alipokutana na waandishi wa habari Machi 13, 1995 katika Hoteli ya Kilimanjaro, Dar es Salaam, alipokuwa anazungumza masuala malimbali ya nchi.

Katika mkutano huo Mwalimu aliweka bayana nyufa tano zilizokuwa zimeanza kuonekana katika nchi ambazo ni, Muungano, Kutojali Katiba ya Nchi, Rushwa, Ukabila na Udini.

Nimeamua kuitoa mifano hii kutokana na mijadala inayoendelea katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na maoni ya watu mbalimbali hasa baada ya kifo cha Hayati Rais John Mgufuli. Ukisikiliza vizuri maoni na michango wa wabunge, utagundua kwamba kuna maoni ya pande mbili. Wafuasi wa Hayati Magufuli upande wa pili ni wafuasi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

CCM miaka yote ambapo wabunge wa vyama vya upinzani wamekuwapo bungeni, walionekana wamoja na imara katika kuchangia na kupitisha hoja. Zaidi ilionekana kwamba wapinzani ni kikwazo cha maendeleo na kwamba ili tuendelee zaidi ni kuhakikisha hawarudi ni ikawa hivyo. Wakati wanafanya hivyo, walijiita "sisi" na wapinzani wakaitwa wao. Kilichokuwa kinawafanya CCM wajiite sisi ni uwapo wa upinzani sawasawa na Wazanzibari au Watanganyika ndani ya Muungano.

Leo CCM ni kama imebaki pekee bungeni na tumeanza kuona mgawanyiko wa waziwazi. Wengi wanafikiri tatizo ni kifo cha John Magufuli lakini kimsingi mgawanyiko huo unatokana na CCM kubaki kama ndio peke yao bungeni. Uhakika nilio nao kama jambo hili lingelitokea wakati wabunge wa upinzani wakiwapo bungeni kama miaka yote, mgawanyiko huu ndani ya CCM usingeonekana kwa maana wote wangelikuwa wanaona tatizo lao ni upinzani. Hoja isingekuwa Magufuli au Samia.

Katika maneno yake, Mwalimu Nyerere alisema: "Ukishakuwa na dhambi ya ubaguzi haitakuacha salama. Mnaweza kujiona wamoja kwa sababu umoja huo umeunganishwa na yule mnayemuona ni adui yenu, yaani adui kawaunganisha. Adui akishaondoka, mkabaki ninyi mtaanza kutuhumiana ninyi kwa ninyi. Msipoangalia mtagawanyika na mwisho mtapasuka kabisa."

Watanganyika ni wamoja kwa sababu wako ndani ya Muungano, vivyo hivyo kwa Wazanzibar. Siku Watanganyika tukibaki wenyewe, kuna uwezekano ndani ya makabila yetu kujiona baadhi tuna maana zaidi kuliko wengine. Kwa sasa unaweza kusikia baadhi ya wana-CCM wakijiita CCM mpya wengine CCM asilia, hii ni kwa sababu hawako ndani ya muungano kwa maana ya kutokuwapo kwa upinzani.

Umoja wa CCM unajengwa zaidi na upinzani imara. Uimara wa CCM unategemea uimara wa upinzani. CCM ikijidanganya kwamba ikibaki peke yake itakuwa imara itapasuka vipande viwili. Kama ambavyo Mwalimu aliifananisha Tanzania na Nyumba nzuri isiyokuwa na nyufa, sasa CCM nyufa zimeanza kuonekana katika kuta, dari na baada ya muda nyumba itaanza kutikisika na pengine nyufa zitaanza kuonekana kwenye msingi na kama nyufa hizo hazitazibwa basi kuna uwezekano mkubwa wa nyumba kubomoka.

Miaka mitano ambayo haikuwa na upinzani, ingetumika kupima nini cha maana kimefanyika au nini kisingefanyika kama upinzani ungelikuwapo. Tathimini hiyo inaweza kuamua ama kuruhusu upinzani au kutoruhusu pamoja na kwamba ni ukiukwaji wa sheria kuamua kama viwapo au visiwapo kwa sababu katiba iko wazi, kwa mtu kujiunga na chama cha siasa anachokitaka.

Mwisho, tusipokubali kwamba umoja wa wana-CCM na CCM yenyewe unatokana na kuwapo kwa vyama imara vya upinzani, basi tutakuwa tumekubali kuivunja CCM vipande viwili. Maneno haya inawezekana leo yasieleweke kwa urahisi mpaka itakapotokea lakini nawaambieni CCM ikiendelea kudhani kwamba kubaki pekee itajenga umoja, itavunja umoja.

Sababu yake ni kwamba, yeyote atakayekuwa anatoa maoni tofauti na ya mwingine, ataonekana msaliti. Vinginevyo CCM ikubali kuwa na wanachama kasuku watakaokubali kuitikia kila jambo bila kuhoji, kitu ambacho hakitakuwa rahisi kwa wanachama makini.

Matatizo tuliyonayo si upinzani wa vyama, ni umaskini, ujinga, maradhi, rushwa na ufisadi. Hayo yakitibiwa, upinzani utaamua wenyewe kuwapo ama kutokuwapo, lakini upinzani hautafutika kama hayo yote yataendelea kuwaandama Watanzania.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Unalikumbuka disco la spika kwenye mtungi?



Na Adam Fungamwango

MAISHA wanakwenda kasi sana. Hivi sasa disko zinatumia vyombo vingi na vya kisasa. Muziki wa disko ukipigwa unaweza kusema kuwa labda kuna dansi linapigwa laivu.

Kwa sasa kuna vyombo ambavyo vinafanya muziki uwe na sauti kubwa zaidi na nzito, kiasi kwamba unaweza hata kukuzibua masikio.

Disko la sasa liwe kwenye kumbi za starehe, harusi, ubatizo, kipaimara ya sherehe zingine za kijamii, linaweza kupigwa sehemu lakini watu waliokuwa kilometa nyingi mbali wakasikia.

Ni kwa sababu ya teknolojia kuzidi kukua. Kila kukicha wataalamu wanatengeneza vyombo ambavyo vitaufanya muziki uvutie zaidi. Ndiyo maana zamani muziki ulikuwa uko kwenye mfumo wa mono, lakini baadaye wataalam wakatengeneza vifaa ambavyo muziki ukawa unasikika kwenye mfumo wa stereo.

Mono ni mfumo wa sauti ambayo inasikika bila kuchujwa. Kama ni muziki unasikika jinsi ulivyo bila sikio kuchambua kama kuna vyombo gani vinapigwa, au sauti.

Mfumo wa stereo inaonyesha sauti iliyochujwa. Wanamuziki wenyewe wana msemo wao kuwa 'imeondolewa mafua' Sauti ya mono wanaiita yenye mafua. Hata muziki ukisikika kwa mfumo wa stereo msikilizaji atasikia sauti nyororo, na vyombo vilivyotumika vikijipambanua na kusikika vizuri kabisa.

Wataalam siku zote hawalali. Wakaendelea kuumiza kichwa ndipo walipogundua kuongeza vifaa vya kuongeza sauti kama vile 'booster Amplifier', 'subwoofer amplifier', na vingine vingi vinavyofanana na hivyo.

Hata redio za kisasa maarufu kama 'sabufa' zina sauti kubwa, nzuri, zilizochujwa na mpangilio mzuri wa besi, kiasi cha hata kuchezesha disko. Zamani haikuwa hivyo. Ni kweli vyombo vya muziki vilikuwa na sauti, lakini hazikuwa na mfumo mzuri kwenye mpangilio au mfumo wa besi.

Sasa hebu tuhame na kurudi miaka mingi nyuma ambapo watu walipokuwa wakitaka kufanya sherehe za kijamii, iwe za kumaliza shule, chuo, harusi, au disco tu la kawaida.

Achana na zile disco za kwenye kumbi. Nalozungumzia mimi ni lile la mitaani na vijijini. Mashine moja ya muziki maarufu wakati huo kikitwa 'record Player', ndiyo iliyokuwa inatumika.

Ni kitu mfano wa sanduku ambacho kilikuwa kinazungusha santuri iliyorekodiwa na bendi mbalimbali za muziki. Sanduku hilo lilikuwa likifunikwa na spika zake mbili. Zile spika zilikuwa na sauti, lakini zilikuwa na stereo sana, lakini hazikuwa na besi.

Kama muziki unasikilizia nyumbani wala haikuwa na tatizo. Lakini kama ni sherehe na hakukuwa na chombo kingine cha kupiga disko, basi 'player' ilifanyiwa utaratibu itoe sauti kubwa zaidi ya ila ya kawaida.

Hapo ndipo utatafutwa mtungi mkubwa, na kile kisanduku cha spika ya kwanza ikawekwa ama juu ya mtungi au ndani, itatengemea na mtaalam mwenyewe atakavyoweza kuiseti. Lengo hapo ni kupata mdundo wa besi ili kunogesha au kupata ladha halisi ya wimbo, pamoja na kuchezeka kwa raha.

Muziki bila besi ni kama chakula bila chumvi, ndimu, pilipili au kachumbari. Na kweli spika ikiingizwa kwenye mtungi na muziki ukianza kupigwa sauti ya besi inasikika kutokana na sauti ya muziki kuzongwa mtungini.

Kuna 'player' zenye spika moja, lakini pia zipo ambazo zina spika mbili. Sasa hizi moja itawekwa kwenye mtungi na nyingine juu ya mti.

Ile inayowekwa juu ya mti lengo lake ni kwamba wote waliokuwa hapo wausikia muziki. Ikikaa chini na kwa vile kuna mkusanyiko wa watu, basi watu wa pande zingine hawata usikia vizuri.

Spika inapandishwa juu ya mti, unafungwa, disco linaanza. Sababu nyingine watu wa mbali kidogo nao waonje ladha ya muziki wa kwenye disko hilo. Hayo ndiyo yalikuwa na mahesabu, ufundi na ujanja na vijana wa miaka ya 1960, 1970, 1980, hadi 1990 mwanzoni.

Hili sasa ndiyo lilikuwa linaitwa 'disko vumbi' maana watu kutoka sehemu mbalimbali au vijiji mbalimbali walimiminika kujumuika kwenye sherehe hizo. Wanapotoka hapo ni vumbi tu mtindo mmoja, miguuni, kichwani hadi kwenye kope.

Ilipofika katikati ya miaka ya 1990, redio kaseti kubwa, zenye maspika makubwa zilianza kuingia nchini na kuchukua nafasi ya 'player'. Zenyewe sasa zilikuwa na sauti kubwa zaidi. Ziliboreshwa na kuwa na besi, pamoja na vifaa vya kuchuja sauti na kutaka kuifanya vyovyote unavyotaka.

Hapa ndipo yalipokuja mageuzi ya kutoka kwenye 'record player' hadi kwenye redio kaseti. Na hata mauzo ya santuli yalianza kupungua, kwani watu walinunua kanda za kaseti badala yake. Kila mwenye pesa sasa alitaka kumiliki redio kaseti badala ya 'player'.

Hata hizo redio kaseti zenyewe muda wake ulipokwisha watu waliziweka pembeni na kifaa kinachoitwa 'music system' kilianza kuchukua nafasi yake. Mpaka sasa redio za aina hiyo zipo. Ila 'subwoofer', maarufu kama 'sabufa' nazo kwa sasa zipo kwenye chati.

Kwenye disko mitaani kwa sasa zinasimamishwa spika kubwa na Ma-DJ wa kisasa wana mashine maalum za kupigia disco, na wengine wana kompyuta mpakato maarufu kama 'laptop' ambazo wanakuwa wamezihifadhi nyimbo zao. Disko likipigwa hadi mtaa wa 12 wanasikia.

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald. Kijana msomi aliyetoka Marekani, anarejea Tanzania. Akakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya Mapenzi-2

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

DAKIKA kumi baadaye simu iliita mezani kwake. Aliiangalia kwa uchungu. Alidhani kuwa Sajenti Peter.

"Mkuu tunapenda kukufahamisha kuwa simu ile ilipigwa maeneo ya Posta, Dar es Salaam. Kwa bahati mbaya sana imepigwa na mteja kwenye kibanda cha simu." Simu ilipokatwa alicheka kicheko kifupi ambacho hakikuwa halisi. Hata mwenyewe hakujua ni cha nini.

Alichoambiwa alikitegemea. Hakuwa mmoja wa watu ambao wanapiga simu ovyo na kulisumbua Jeshi la Polisi. Huyu alikuwa anajua anachokifanya.

Hakupiga simu ya mkononi. Na wala hakupiga simu kwa kutumia simu ya mezani ikiwa nyumbani. Alijua atapatikana. Na wala hakutaka kwenda kibanda cha simu ya mitaani.

Aliamua kwenda Posta ambako kuna mkusanyiko wa watu wengi.


Kwa maana hiyo alitegemea kitu kibaya kutokea dakika si nyingi zijazo.

Simu iliita tena, akainyanyua mkono. "Afande nipo kwenye eneo la tukio. Niko wa wenzangu wa kituo kidogo cha polisi cha jirani hapa. Ni kwamba maeneo ya Afrikana tumeukuta mtu amefariki. Ni mwili wa mwanamke ambaye ana miaka kuanzia 23 hadi 26 hivi afande. Ulionekana alfariji kwenye mtaro. Kwa mujibu wa watu hapa wanadhani kwamba huenda ni mmoja wa wanawake makahaba na inawezekana amegongwa na gari, au ameuawa, hilo nadhani litajulikana baadaye uchunguzi utakapofanyika afande."

Ilikuwa ni taarifa fupi ya awali kutoka kwa afande Peter, lakini inayojitosheleza kwa wakati huo.

Inspekta Andrew mpaka wakati huo hakushangazwa na taarifa ya kuokotwa kwa maiti ya mwanamke. Alishaambiwa kuwa kuna zawadi yake na mtu huyo 'muuaji mjivuni'.

Yeye ameshatambua kuwa hayo ni mauaji. Ni kwa sababu ametaarifiwa na mtu aliyeonekana amefurahia kifo hicho. Kitu ambacho ameshangazwa kidogo ni jinsi msichana huyo alipotupwa kwenye mtaro na lengo lionekanane kama




**"Mkuu tunapenda kukufahamisha kuwa simu ile ilipigwa maeneo ya Posta, Dar es Salaam. Kwa bahati mbaya sana imepigwa na mteja kwenye kibanda cha simu." Simu ilipokatwa alicheka kicheko kifupi ambacho hakukuwa halisi. Hata mwenyewe hakujua ni cha nini.**

amegongwa na gari.

Kama isingekuwa sauti ya yule jamaa, inawezekana kila mmoja angejua huenda mwanamke huyo amegongwa na gari.

Ambacho kwa sasa anachosubiri ni taarifa tu ya madaktari ili kazi ianze na kufuatilia ni nani wamehusika kwenye mauaji hayo na pia kumfutilia mtu ayepiga simu kuitaarifu polisi juu ya mauaji hayo na anahusika vipi.

*****************************

"Pamoja na yote hayo ambayo nimekwambia mimi, lakini pia kuna jambo la mwisho ambalo mama yako atakushauri." Alimaliza mzee Peterson.

Kilikuwa ni kikao kifupi yeye, mkewe Eva na kijana wao wa pekee Donald.

"Nashukuru Baba na Mama kwanza kwa kunizaa. Kunilea. Kunisomesha. Tena kunipa elimu ya juu mpaka kwenda kusoma nchini Marekani na kupata shahada ya juu ya biashara. Kwa roho moja nimekubali kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa makampuni yetu ambayo baba uliyaanzisha kwa tabu, lakini sasa yamekuwa mfano kwa makapuni mengine nchini Tanzania. Naahidi nitaendeleza pale ulipoishia na kuendelea kupaisha bidhaa zetu zaidi na zaidi." Donald aliongea kwa unyeyekevu.

Kilikuwa ni kikao cha kifamilia, lakini pia cha kibiashara. mzee Peterson ambaye ni mmiliki wa kampuni ya PIG alikuwa na mpango wa kumpa cheo cha Ofisa Mtendaji Mkuu. Na hii ni baada ya wiki chache zilizopita kutoka masomoni Marekani.

Mzee Peterson aliamua kumsomesha kijana wake masomo ya biashara kwa makusudi ili aje kuwa mrithi zake kwenye kampuni yake. Hakutaka tena kuajiri Maofisa Watendaji Wakuu. Alitaka kijana wake aanze na cheo hicho, ili hata ikitokea akafariki dunia awe na uwezo wa kuiendeleza mali.

Mzee Peterson alitaka sehemu zote muhimu za kampuni ziongozwe na familia. Yeye kama mmiliki alijipa cheo cha Mkurugenzi Mtendaji, mkewe Eva ni Ofisa Uzalishaji mali na masoko. Tatizo lilikuwa kwenye cheo cha Ofisa Mtendaji Mkuu. Waliajiri mtu. Alifanya kazi vizuri, lakini hawakuridhika. Walikuwa wanamsubiri Donald amalize masomo yake ili aje kuchukua cheo hicho. Sasa walikuwa wamekamilika.

"Sasa ujiandae. Jumatatu tutakwenda ofisini nikakutambulishe rasmi kuwa wewe ndiye Ofisa Mtendaji Mkuu mpya."

"Sawa Baba."

"Kingine mwanaNgu." Eva alidakia. na kukaa kimya kwa sekunde chache.

Donald alimkodolea macho mama yake. Alihisi kuwa anachotaka kuongea hakihusiani tena na mambo ya kazi kwenye kampuni yao.

"Unakwenda kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni. Unahitaji kuwa na heshima na kuheshimiwa. Una miaka 30 sasa, unatakiwa uwe na mke uoe."

Ni kitu ambacho hakikutilia maanani sana kwenye akili yake. Lakini kwa sababu waliomshauri na wazazi wake alijikuta akikubali.

"Sawa mama, lakini sidhani kama itakuwa haraka haraka hivyo." Donald alimjibu mama yake huku baba yake akiwa hajatia neno lolote.

"Inaweza ikawa hivyo, lakini pia inaweza kuwa haraka. Kwa sababu kule kwa shangazi yako nimemuona

ITAENDELEA JUMAPILI



# LULU APANGA ATAKAVYOLEA WATOTO

MWIGIZAJI anayetamba katika filamu za Bongo, Elizabeth Michael, maarufu kama Lulu, amesema akipata watoto atawaacha huru waishi maisha ya kawaida kama alivyo yeye mwenyewe.

Lulu amesema kama mzazi ataangalia namna ya kuwalea kwa maadili na hata matumizi ya mitandao ya kijamii atawapa mpaka kulingana na umri wao kutokana na athari zake kuwa nyingi kuliko faida.

"Kiukweli hata mimi inshaallah nikijaaliwa watoto, watu watawaona shuleni, cliniki au barabarani yaani sitawaficha ila watawaona kwenye maisha ya kawaida tu. Kuhusu mitandaoni huku tupambane wenyewe tu, lakini kama mtoto atafika umri wa kuamua anataka nini sawa wazazi tunapaswa kusaidia kwa mipaka fulani," amesema.

## Makabila ulitumwa kuwachokoza Yanga?

MWANAMUZIKI wa singeli, Dula Makabila, amepigwa mkwara na mashabiki wa Yanga, wakisema hawatamsamehe kwa kitendo chake cha usaliti.

Shabiki na Mwanachama wa Klabu ya Yanga, Jimmy Kindoki, amempa onyo msanii huyo kwa kumtaka asirudi tena kuishabikia timu yao baada ya kutangaza kuhamia Simba.

"Ole wako tusikie umerudi Yanga ndio utajua siku hiyo kama Yanga ina wenyewe, mmekosa kiki kwenye muziki wenu sasa mnahamia huku, nikwambie tu hiyo furaha ya Simba ni ya muda mfupi siku huyo Moo akisema basi ujue Simba inarudi kwenye msoto" amesema.



## Mbosso wa Bongo hadi Marekani

MSANII anayekonga watu kwa nyimbo za mahaba, Mbosso, ameanza kuitangaza Album yake mpya Definition Of Love' kimataifa.

Uzidunzi wa albama hiyo ulipangwa kufanyika Machi, lakini kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais, Hayati John Pombe Magufuli, iliahirishwa na inatarajiwa kufanyika mwezi unaokuja.

Katika kile kinachoonekna maandalizi yake ni makubwa, tangazo la Album hiyo limeonekana katika skrini zilizopo katika eneo maarufu la Times Square huko jimbo la New York.



# Mourinho: Sitojali kuhusu Pogba

**LONDON,** England

KOCHA Mkuu wa Tottenham, Jose Mourinho amesema kuwa hawezi kujali kuhusu yale ambayo anayasema kwa sasa kiungo wa Manchester United, Paul Pogba, kuwa yeye ni mkosoaji.

Pogba aliwahi kufundishwa na Mourinho katika kikosi cha Man United na walikuwa na mvutano wa mara kwa mara kabla ya kocha huyo kufutwa kazi na sasa United ipo chini ya kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Kiungo huyo hivi karibuni alisema kuwa Mourinho alikuwa anatoa maelekezo na kukosoa pale ambapo wanashindwa kufanya, jambo ambalo ni tofauti na kocha wao wa sasa namna anavyofanya kwa kuwa anakwenda nao sawa.

Pia kutokana na tofauti zao Mourinho alimvua kitambaa cha unahodha Pogba jambo ambalo liliongeza mvutano wake.

Baada ya sare ya Tottenham kufungana mabao 2-2 dhidi ya Everton juzi Ijumaa, Mourinho amesema kuwa ni masuala yake anayofikiria.

Mourinho alipotakiwa kutoa maoni yake kuhusu maneno ya Pogba kupitia Sky Sports alisema:"Ninapenda kusema kwamba sijali kuhusu ambacho amekisema, sijavutiwa nacho katika yote."

Pogba aliweza kunyanyua taji la Ligi na Ligi ya Europa katika msimu wa kwanza wa kufanya kazi na Mourinho ndani ya Man United.





# RONALDO YUPO SANA JUVE - PEPE

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo ana furaha pale Juventus na anaonekana akataa kwa miaka mingi, kwa mujibu wa mchezaji mwenzake wa zamani wa Real Madrid na Ureno, Pepe.

Fowadi huyo amefunga mabao 25 kwenye mechi 27 za Serie A msimu huu, akiongoza orodha ya wafungaji kwa tofauti ya mabao manne dhidi ya Romelu Lukaku.

Ronaldo amekuwa na kiwango bora tangu umesajili na Juve kutoka Real Madrid mwaka 2018 na kuendelea kuwa vizuri katika umri wake wa miaka 36, na sasa amebakisha mabao matatu kufikisha 100 kwa klabu hiyo ya Italia kwenye mashindano yote.

Hata hivyo, majaliwa ya mchezaji huyo pale Juventus yamekuwa shakani baada ya timu yake kuondolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 na timu ya Porto ambayo Pepe anaichezea.

Pia kwenye mbio za Ligi Kuu, Inter Milan inaonekana kuwa kwenye nafasi nzuri zaidi ya kutwaa ubingwa na Ronaldo amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka klabuni hapo.

Lakini Pepe anafikiri Ronaldo ataendelea kuwapo kwenye kikosi cha Juventus kwa miaka mingi.

Pepe aliulizwa kama Ronaldo atarudi kucheza soka nchini Ureno alikoanzia kucheza soka la kulipwa na Sporting CP.

Aliiiambia Novo: "Kiukweli kwa jinsi ninavyomfahamu yeye, naamini atabakia pale na hawezi kurudi Ureno.

"Nafikiri ana furaha kule Turin. Yeye ndio anaongoza kwa ufungaji bora kwenye Serie A. Wote wanaomshutumu hawajui ugumu wa kufunga mabao."

# *Rais PSG anaamini watabeba Uefa*

**PARIS,** Ufaransa

RAIS wa Paris, Saint Germain, Nasser Al Khelaifi, amesema kuwa ana matumaini ya klabu hiyo kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na kwamba nyota wake wawili, Neymar Jr na Kylian Mbappe watabaki kikosini hapo.

PSG imefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya ligi ya mabingwa Ulaya baada ya kuwaondoa mabingwa watetezi, Bayern Munich.

Rais huyo amesema:"Tumewekeza sana kuona kwamba tunafanikiwa na kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja na makombe mengine.

"Kama tumewekeza sioni sababu ya Neymar na Mbappe kuondoka hapa kwa sababu tuna kila kitu na tunatakiwa kushinda kila kitu.

"UEFA bado haijamalizika ila tunatakiwa kupambana na msimu huu tuweze kufanya kitu cha tofauti," .

Mbappe alikuwa anatajwa kuibukia Real Madrid huku Jr yeye alikuwa anatajwa kuibukia ndani ya Barcelona.



# DONDOO SOKA
## MAGAZETI ULAYA




# LAPORTA: MESSI ATABAKI CAMP NOU

## ●●● Asema atafanya kila linalowezekana kuhakikisha anasaini mkataba mpya na...

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, "anaamini" Lionel Messi atasaini mkataba mpya wa kubakia kwa miamba hao wa Ligi kuu ya Hispania, LaLiga.

Messi mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu na nyota huyo mwenye umri wa miaka 33 majaliwa yake bado hayajulikani huku akihusishwa na Paris Saint-Germain na Manchester City.

**Laporta bado anaamini kwamba, Messi, ambaye ametumia muda wake wote kucheza hapo Camp Nou atasaini mkataba mpya.**

Wakati Barca jana walikua wakicheza na Athletic Bilbao kwenye fainali ya kombe la Copa del Rey, Laporta aliulizwa kuhusu mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or.

"Kila kitu kinakwenda sawa," alisema Laporta akiiambia Deportes Cuatro.

"Nitafanya kila kitu ndani ya uwezo wangu kuhakikisha anabakia hapa. Na hicho ndio tunachokifanya kwa sasa. Messi anahamasika.

"Ni mtu wa kawaida na ninashawishika kwamba, ataendelea kubakia hapa Barca."

Messi amefunga mabao 23 kwenye Ligi na kutoa pasi za mwisho 28 katika LaLiga msimu huu.

Kwa ujumla, Messi amefunga mabao 29 kwenye mashindano yote kwa msimu huu 2020-21.

## ZISIKUPITE

### RICE AWANIWA MAN UNITED

KLABU ya Manchester United inatathmini uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa England, Declan Rice, 22, katika mkataba kati yao na West Ham utakaomhusisha Jesse Lingard, 28. ***(Athletic - subscription required)***

### LEEDS WAMTAKA AGUERO

KLABU ya Leeds United imejiunga na kinyang'anyiro cha kuwania kumsajili mshambuliaji wa Manchester City na Argentina, Sergio Aguero, 32, ambaye mkataba wake unakamilika mwisho wa msimu huu. ***(90min)***

### MBAPPE AKATAA

HATIMA ya mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe, 22, katika klabu ya Paris St-Germain haijulikani baada ya nyota huyo kukataa kusaini mkataba mpya. ***(Telegraph - subscription required)***

### VINICIUS CHAMBO KWA MBAPPE

REAL Madrid wanajiandaa kumtumia mshambuliaji wa Brazil, Vinicius Junior, 20, katika mkataba wa kumsajili Kylian Mbappe msimu huu wa joto. ***(El Chiringuito, via Metro)***

### VAZQUEZ HAJUI HATIMA

WINGA wa Real Madrid, Lucas Vazquez, 29, ambaye mkataba wake unamalizika mwisho wa msimu huu, hajaamua kuhamia yake pale Bernabeu, huku Manchester United na Chelsea wakionesha nia ya kutaka kumnunua. ***(Sun)***

### BEI YA ANDERSON YATAJWA

LYON wameweka euro milioni 25 kama bei ya awali ya kumuuza mchezaji wao, Joachim Andersen, 24, ambaye yuko Fulham kwa mkopo. Manchester United na Tottenham zinamnyatia. ***(Metro)***

### JUVE KUMRUDISHA KEAN

JUVENTUS inataka kusajili tena mshambuliaji wa Everton na Italia, Moise Kean, ambaye anacheza kwa mkopo kule Paris St-Germain. Everton wanataka euro milioni 50 kwa ajili ya kumuachia nyota huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Gazzetta)***

### CHELSEA NA WACHEZAJI

CHELSEA wanaangalia uwezekano kubadilishana wachezaji kati ya Alex Sandro, 30, kutoka Juventus na Emerson Palmieri mwenye umri wa miaka 26 kwenda kule Turin. ***(Calciomercato)***

### BERNARD ATAKIWA REAL BETIS

WINGA wa Everton, Bernard, 28, anawaniwa na kocha wa Real Betis, Manuel Pellegrini na anataka kumsajili wakati wa dirisha la uhamisho la kipindi cha majira ya joto kinachokuja. ***(Fichajes)***

### VILLA NA BARKLEY

ASTON Villa wameiambia Chelsea kuwa hawana haja na mkataba wa kudumu na kiungo wa kati wa England, Ross Barkley mwenye umri wa miaka 27 ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo. ***(TEAMtalk)***

HABARI MICHEZO

## Gwambina yalia na nyasi bandia Uhuru

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Gwambia FC, Mohamed Badru, amesema kuwa pamoja na makosa ya safu yake ya ulinzi kuruhusu mabao matatu kwenye mechi dhidi ya KMC, lakini kwa kiasi fulani uwanja wenye nyasi bandia utakuwa umechangia kwa sababu ni mara ya kwanza kwao kuuchezea.

Akizungumza juzi baada ya kuchapwa mabao 3-0 dhidi ya KMC ya Kinondoni, Uwanja wa Uhuru, Dar es salaam, kocha huyo alisema kuwa kwenye mechi hiyo ameshindwa hata kutengeneza nafasi kutokana na aina ya uwanja na jinsi alivyowaandaa wachezaji wake kucheza.

"Sikudhania kama itakuwa hivi. Lakini hongera kwao KMC, wamecheza vizuri na wazoefu kwenye uwanja huu na wametumia makosa ya walinzi wangu ambao walikuwa wanajirudia," alisema Badru.

Hata hivyo alisema kuwa makosa ambayo ameyaona atakwenda kuyarekebisha kabla ya kuwavaa Yanga siku ya Jumanne.

Kwa upande wa KMC, Kocha Msaidizi Habib Kondo, alisema kuwa walicheza kwa tahadhari kubwa hasa kipindi cha kwanza kutokana na mechi yao iliyopita Gwambina kuishindilia Coastal Union mabao 4-0.

Yalikuwa ni mabao ya Charles Ilamya dakika ya 51, Emmanuel Mvuyekure, dakika ya 62 na Ally Juma dakika ya 71.

## Gekul aishuruku JICA kuinua riadha

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Habari,Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul amelishukuru Shirika la Kimataifa la Maendeleo la nchini Japan (JICA), kwa kutoa msaada wa vitabu 120 kwa ajili ya wanariadha.

Akizungumza katika hafla iliyofanyika juzi mbele ya viongozi wa Baraza la Michezo Tanzania (BMT) na Shirikisho la Riadha Tanzania, Gekul alisema anaishukuru

JICA kwa kuendelea kuiunga mkono Serikali katika sekta ya michezo hususani mchezo wa riadha.

Gekul alisema JICA wamekuwa wadau wakubwa katika kuendeleza mchezo wa riadha hapa nchini ambapo kwa zaidi ya miaka mitatu sasa wamedhamini mashindano ya riadha kwa wanawake pamoja na kutoa utaalamu.

"Serikali inatambua suala la michezo ni ajira, kazi na afya hivyo tutasimamia na kutatua changamoto wanazozipata vyama vya michezo ili kuendeleza michezo kwa taifa letu," alisema Pauline.

Aidha Gekul ameitaka RT kuhakikisha viatu hivyo vinatolewa kwa watu sahihi pamoja na kushirikiana vyema na Taasisi ya JICA kuandaa mashindano mbalimbali nje ya Dar es Salaam ili kuibua vipaji vipya vya wanariadha hususani kwenye mikoa yenye vipaji vya riadha.

# KOCHA KMC APANIA NNE BORA LIGI KUU

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Habibu Kondo, amesema kuwa kwa sasa wamejipanga kuhakikisha wanapata pointi tatu kila mechi ili kufikia malengo ya kumaliza kwenye nne bora katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Akizungumza baada ya mchezo huo wa ushindi wa 3-0 uliopigwa kwenye uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi, Kondo alisema wamejipanga kuhakikisha wanamaliza kwenye nafasi hiyo.**

Kondo alisema malengo yao ni kuhakikisha wanamaliza katika nafasi nne bora hivyo analazimika kupambana ili kutafuta pointi muhimu katika kila mechi iliyopo mbele yao.

"Hatuwezi kufikia malengo yetu hadi kupata kupata matokeo mazuri ya mechi, hivyo tulitegemea pointi tatu kwa Yanga tulifanikiwa moja, tulijipanga dhidi ya Gwambina kwa bahati nzuri tumezipata na kutuweka katika nafasi nzuri," alisema Kondo.

Alisema kipindi cha kwanza alichukua muda kuwasoma Gwambina na kutumia upungufu wao kipindi cha



pili na kufanikiwa kupata idadi ya mabao 3-0 na sasa wanajipanga na mechi ijayo.

Naye Badru alisema kushindwa kujiamini kwa wachezaji wao pamoja na kutoyafanya yale aliyowaambia katika mazoezi imewafaidisha KMC FC kupata idadi kubwa ya mabao katika mchezo huo.

"Wachezaji wangu hawakutekeleza kile nilichowaambia walushindwa kujiamini na KMC FC waliingia kwa kujiamini na kutumia mapungufu yetu kutufunga bao 3-0 na kupata pointi tatu kwenye uwanja wao wa nyumbani," alisema Badru.



Mchezaji wa timu ya mpira wa Wavu ya JKT 836, Jesca Peter, akipiga mipira kuurudisha kwa timu pinzani ya Chui, katika michuano ya mpira wa wavu ya Muungano yanayoendelea katika Uwanja wa Ndani wa Taifa juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ligi soka Wanawake Aprili 23

**Na Saada Akida**

BAADA ya kusimama kwa muda mrefu, ligi kuu ya Wanawake Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea Aprili 23, mwaka huu, huku viwanja vitatu vikiwaka moto kwa JKT Queens ikiwakaribisha Kigoma Sisterz katika dimba na Meja Jenerali Isamuyo jijini Dar es Salaam.

Michezo mingine itakayopigwa siku hiyo ni TSC Queens wakiwa nyumbani kwao na kuwakaribisha Mlandizi Queens, kwenye uwanja wa CCM Kirumba uliopo Mwanza na Tanzanite SC dhidi ya Mapinduzi Queens uwanja wa Fountain Gate Arena.

Aprili 24, mwaka huu mabingwa watetezi na vinara wa ligi hiyo, Simba Queens itakuwa ugenini wakisaka pointi muhimu dhidi ya Alliance Girls katika dimba la Nyamagana, Mwanza.

Katika tarehe hiyo Yanga watakuwa na kibarua nyumbani katika uwanja wa Karume, jijini Dar es Salaam ikiwakaribisha ES Unyanyembe na mchezo mwingine dhidi ya Baobab Queens ya Dodoma ambao watakuwa nyumbani ikiwakaribisha Ruvuma Queens kwenye uwanja wa Jamhuri.

Timu hizo ambazo zimekamilisha michezo 15 ya mzunguko wa kwanza huku Simba ikiongoza msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 39, wakifuatiwa na Yanga yenye alama 38 nafasi ya pili na JKT Queens nafasi ya tatu pointi 36.

Alliance Girls wakiwa nafasi ya nne wakikusanya pointi 28, Ruvuma Queens ikiwa nafasi ya tano wa alama 25 na nafasi ya sita ikishikiliwa na Mlandizi Queens kwa pointi 23 wakiwa sawa pointi na Baobab walikuwepo nafasi ya saba.

Nafasi ya nane ikishikiliwa Tanzanite SC kwa alama 19, TSC wakiwa nafasi ya tisa kaa pointi 14, Kigoma Sisterz ikiwa nafasi ya 10 kwa pointi 12, Mapinduzi Queens ikiwa nafasi ya 11 kwa alama tatu ikishinda mechi mmoja na ES Unyanyembe ikiburuza mkia ikiwa nafasi ya 12 kwa kutokuwa na pointi yoyote kwenye michezo 15 ya ligi hiyo.

# Michezo

Jumapili Aprili 18, 2021

Nipashe




Laporta: Messi atabaki Camp Nou UKURASA 22



Kipa wa timu ya Gwambina FC, Mohammed Husein, akipangua mpira ulioelekezwa golini kwake katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru juzi dhidi ya KMC. KMC ilishinda mabao 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Makipa Yanga wapelekwa bichi

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA mpya wa makipa wa Yanga Razack Siwa amesema alianza kuwapeleka ufukweni makipa wa timu hiyo baada yakugundua kuwa hawakuwa na mazoezi ya kutosha.

Siwa ambaye amechukua mikoba wa kocha wa makipa aliyepita Mrundi, Vladmin Niyonkuru aliyetimuliwa hivi karibuni pamoja na aliyekuwa Kocha Mkuu, Cedrick Kaze, alisema kuwa aliwakuta makipa wa Yanga wakiwa hawana morali na hata bidii yao ilikuwa chini, hivyo kuwaweka sawa kisaikolojia.

Kocha huyo raia wa Kenya alisema kuwa kazi yake ya kwanza ulikuwa kuwapeleka ufukweni kwa ajili ya kuwaweka sawa kwenye stamina za mikoni, miguu na pumzi pia ili waweze kuwa bora wawapo langoni.

"Niliwakuta wapo chini kimorali, hata kwa bidii ilikuwa chini. Nilijaribu kuzungumza nao nikawaambia kuwa kazi ya ukipa ni ngumu sana na ni lazima ujitolee," alisema.

"Tukaanza mazoezi ya kwenda bichi kuwaweka sawa stamina ya mikono, miguu na pumzi. Wiki ya kwanza tulikwenda mara mbili, kwa sasa ligi imeanza tunakwenda mara moja na jioni tunafanya mazoezi uwanjani," alisema Siwa ambaye si mara ya kwanza kuwa kocha wa makipa Yanga.

Alisema kuwa kwa sasa kimazoezi wanaendelea vema na si kama walivyowakuta, lakini bado kuna makosa fulani ambayo wanayo ambayo yatafutika taratibu kadri atakavyodizi kuwapa mazoezi.

"Kuna makosa fulani, lakini hayawezi kuondoka mara moja ila yatafutika tayaribu wakifika pale ambapo mimi nahitaji," alisema.

# Simba kazi kazi kwa Mwadui leo

## ●●● Gomes asema rekodi ya kufungwa 1-0 msimu uliopita imemtisha na sasa...

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza, Simba itacheza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa ugenini tangu Februari 18, mwaka huu, itakapopambana na Mwadui FC kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga.

**Mara ya mwisho Simba kucheza mechi ya Ligi Kuu ugenini ilikuwa Februari 18 ilicheza dhidi ya Biashara United kwenye Uwanja wa karume mjini Musoma mkoani Mara na kushinda bao 1-0 lililofungwa na Benard Morrison.**

Kutokana na matokeo mabaya ya Simba kwenye mechi ya msimu uliopita ya Simba ikicheza kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga ilipofungwa bao 1-0, imemfanya Kocha Mkuu Didier Gomes kwenda na wachezaji wote 28 waliosajiliwa.

Kocha Gomes amesema kuwa rekodi ya kufungwa bao 1-0 kwa timu yake msimu uliopita kwenye uwanja huo imemtisha, hivyo anaichukulia mechi hiyo kwa umakini zaidi.

"Tukitaka kucheza mechi za kimataifa ni lazima kwanza tushinde nyumbani, hii ndiyo njia kwa hiyo ni lazima tuhakikishe tunashinda mechi kama hizi,"alisema kocha huyo.

Kocha Mkuu wa Mwadui, Salhina Mjengwa, amekiri kuwa Simba ni timu bora na timu yake ya Mwadui FC inakwenda kucheza na timu yenye mwendelezo mzuri ndani na nje ya nchi, lakini wao wamejiandaa kikamilifu, huku wakitambua kuwa wapinzani wao wamekuja kwenye uwanja ambao si rafiki.

"Msimu uliopita walipoteza hapa. Kwa hiyo pamoja na ubora wao wanajua kuwa wamekuja kwenye uwanja ambao si rafiki. Ni kweli hatuko kwenye hali nzuri, lakini timu yetu haichezi vibaya kwa hiyo pointi tatu zetu tutaanza kuzipata kwa Simba," alisema kocha huyo ambaye ni mchezaji wa zamani wa Mtibwa Sugar.

Simba itaingia dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kuipa kipigo kinene cha mabao 5-0 timu ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumatano iliyopita.

Kazi itakuwa kwa Mwadui FC ambayo itakuwa inaingia dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kipigo cha mabao 5-0 ilichokipata dhidi ya timu hiyo kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Oktoba 31, mwaka jana.

Mabingwa wao watetezi wataingia uwanjani wakiwa wanatafuta pointi tatu ili kusaka kilele cha msimamo wa Ligi Kuu. Kwa sasa ina pointi 49 na kama ikishinda itafikisha pointi 51, hivyo kujiweka kwenye mazingira ya kuutetea ubingwa huo mara nne mfululizo.

Mwadui yenyewe inashika mkia ikiwa na pointi 16 tu kwa mechi 25 ambazo imecheza mpaka sasa.

Hali mbaya iliyonayo Mwadui, ndiyo itawafanya wapambane kufa na kupona kupata pointi tatu ambazo zitawasukuma kwenda juu na kufikisha jumla ya pointi 19, ingawa hazitoweza kuwafikia Mbeya City iliyo kwenye nafasi ya 17 kwa pointi 21.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >